ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 9 Julai, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Hamad Omar (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea na leo kuna wageni kama kawaida yetu, vijana wetu wanafunzi kutoka skuli mbali mbali wanapendelea sana kuja hapa, ili kusoma mambo yanayohusu nchi yao kutoka kwa Wawakilishi wao.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe leo wageni wetu waliopo pale juu sehemu ya wageni upande wa kushoto yangu pale, ni wanafunzi kutoka Skuli ya Sekondari ya Mwembeladu na jumla yao ni wanafunzi 50 pamoja na walimu wao 3. Kwa hiyo, niwaombe walimu pamoja na wanafunzi wasimame kwa ajili ya kusalimiana na Waheshimiwa Wajumbe, wale pale. Waheshimiwa Wajumbe, hao ndio wanafunzi tulionao leo ni wanafunzi wa Skuli ya Sekondari ya Mwembeladu karibuni sana. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 144

Taa za Mionzi ya Jua Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu naomba uniruhusu kusema yafuatayo. Kwanza nataka nilipongeze Baraza la Manispaa kwa jitihada walizochukua kuweza kung'ara mji kwa taa zinavyopendeza chini ya Waziri wake msikivu Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini. Baada ya maelezo hayo, naomba sana swali langu lijibiwe.

Baraza la Manispaa Zanzibar limefanikiwa kuweka taa za barabarani, ambazo zinatumia mionzi ya jua na kupunguza gharama za umeme.

(a) Je, serikali imetoa elimu gani kwa wananchi na madereva wa magari juu ya usalama wa taa hizo.

(b) Manispaa imeokoa kiasi gani cha fedha walizokuwa wakitumia kwa gharama za umeme baada ya kufungwa kwa taa hizo.

(c) Kwa kuwa teknolojia ya taa hizo ni mpya kwa Zanzibar, Baraza la Manispaa lina mafundi wangapi wa kutengeneza taa aina hizo pale zinapoharibika.

(d) Mradi wa taa hizo umegharimu kiasi gani cha fedha na muda wa matumizi ya taa hizo ni miaka mingapi.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 144 lenye sehemu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

a) Serikali inakusudia kuandaa *program* maalum ya kuelimisha jamii kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar, Asasi za Kiraia na makundi maalum juu ya umuhimu wa utunzaji wa taa za barabarani zenye kutumia nguvu ya jua.

b) Katika kipindi cha mwezi wa Aprili na Mei, ambapo taa hizo ndio zimeanza kuwashwa, serikali imeweza kuokoa jumla ya shilingi 1,065,416.80/=.

c) Mafundi waliopo sasa ni wawili ambao tayari wamepatiwa mafunzo ya matengenezo ya taa hizo endapo zitaharibika kupitia Kampuni ya *ZTE* ambayo ndio ilifunga taa hizo.

d) Mradi wa taa hizo umegharimu jumla ya fedha za Kichina zinazoitwa 5,000.000/= RMB sawa na shilingi 1,300 milioni. Makadirio ya muda wa matumizi wa taa hizo ni miaka 10, kila baada ya miaka mitatu taa hizo zitatakiwa kubadilishwa betri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana aliyotoa Mhe. Waziri.

(a) Kwa kweli hizi taa zimefungwa hivi karibuni na nyengine kuonekana kuwaka na nyengine haziwaki. Je, Mhe. Waziri tatizo nini.

(b) Mhe. Waziri tokea kufungwa taa hizo angalau amefanya ziara wakati wa usiku kwa ajili ya kuzikagua.

Mhe.Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, hivi majuzi tu nilizungumza katika michango ya Waheshimiwa Wajumbe, kwamba tunakiri kweli zipo baadhi ya taa haziwaki, na taa zile ziko chini ya miti, kwa hiyo ile miangaza ya jua haiendi vizuri kama inavyopaswa na hilo tumeliona na tutalirekebisha.

Lakini tumesema kwamba ule mradi bado hatujakabidhiwa rasmi na ulikuwa kwa wajenzi na ule tunasema *Pilot Project*. Kwa hivyo, wenyewe wanataka kuona kwamba mafanikio na matatizo yake, ili marekebisho sawa kwa awamu ya pili waje warekebishe zaidi.

Kuhusu kufanya ziara mimi kila saa 2 mpaka 3 usiku huwa ninafanya ziara mji mzima na ninamualika Mhe. Jaku Hashim Ayoub twende pamoja tupite kwenye vichochoro vyake vya Mchangani. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Kwa kuwa Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekiri kwamba ile ni teknolojia mpya. Vile vile teknolojia ile inafyonza mwangaza wa jua na halafu kuutawanya kuwa muangaza wa kawaida, ambao tunapata nuru ya kuona.

Mhe. Spika, kwa kuwa tumezoea umeme huu ambao ikitokea shoti kuna *controlling unit* au *socket breaker* inakata na shoti ile ikaondoka. Sasa Mhe. Spika, kwa teknolojia hii wakati taa zile hazina *controlling unit* wakati itakapotokea shoti.

Je, haoni kwa kuweka barabarani ikija kutokezea shoti wananchi watakuja kuungua.

(b) Kwa kuwa mradi huu ni mpya, na kwa kuwa anasema kwamba taa nyengine haziwaki kwa sababu ziko kwenye miti na hazipati kufyonza vizuri mwangaza wa jua, hivyo zinashindwa kuwaka. Kwa hivyo, katika kipindi cha masika ambapo jua halipatikani Mhe. Spika, inakuwa mawingu totoro katika mji. Jee, haoni kwamba watatuweka gizani katika kipindi cha Machi, Aprili na Mei wakati mji utakuwa giza, haoni kama teknolojia hii kuwa haifai.

(c) Lini mradi huu Mhe. Spika, utahamia katika kisiwa chengine cha Zanzibar, yaani kule Pemba mpaka Vitongoji kule kwangu mimi utafika lini mradi huu. *(Makofi)*

Mhe.Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa kweli maswali haya nafikiri Mhe. Mjumbe angempa mtaalamu wa umeme kuliko kwa Waziri, kwa sababu yako *very specific* kwenye utaalamu. Sasa Mhe. Spika, mimi sipendi kubahatisha acha tuyachukue na tukayafanyie kazi vizuri na baadaye tuje tumpe majibu. *(Makofi)*

Lakini ninachotaka kusema ni sababu moja ile tuliyosema ya matawi hiyo ndio imeonekana tatizo moja wapo, lakini pengine kuna matatizo ya *battery*. Kwa hivyo, ndio kama nilivyosema bora kwa sababu yamekuwa *very specific* kitaalamu zaidi na mimi sitaki kuji-*commit* kwa hilo.

Mhe. Spika, nadhani ni vyema nijibu la mwisho kuhusu barabara za Pemba. Kwa kweli tayari tumeshasema kwamba tunamalizia hii *Pilot Project* kwa Unguja na halafu kwa Pemba tutaanza Chake Chake, mipango iko tayari wamesha-*survey* na *Inshaallah* tutaanzia hapo na kidogo kidogo tumalize.

Napenda kusisitiza tena Mhe. Spika, kwamba tumesema ni *Pilot Project* na Mhe. Mjumbe yeye ni mtaalamu sana na anajua nini maana ya *Pilot Project*. Kwa maana hiyo, tunatizama mafanikio, matatizo, ili turekebishe vipi na halafu tuendelee.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, swali ambalo nimeliuliza la nyongeza ni muhimu sana, ambalo Mhe. Waziri anasema linahitaji watu wa *technicians*. Kwa hivyo, ni lini atanijibu baada ya kuwasiliana na wataalamu wake, atanijibu humu ndani ya Baraza au kwa maandishi, ili wananchi waone kama huu umeme hauna tatizo, kwa sababu wanaweza kuja kuzikimbia hizi taa. Mhe. Spika, nadhani ni vyema tuwatoe wasi wasi wananchi, hivi Mhe. Waziri atanijibu humu ndani au kwa maandishi na lini.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, lete majibu haraka iwezekanavyo.

Mhe.Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nitajitahidi kumpatia jawabu ndani ya wiki moja. (*Makofi*)

Nam. 44

Matengenezo ya Uwanja wa Amani

Mhe. Nassor Salim Ali – Aliuliza:-

Kwa kuwa sherehe za miaka hamsini ya kusherehekea Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964, serikali imekusudia kupanga sherehe kubwa na hali ya uwanja wa Amani sio nzuri ukizingatia ukubwa wa sherehe hizo.

Je, wizara inajipanga vipi kuufanyia matengenezo uwanja huo wa Amani kwa ajili ya sherehe hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii, na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 44 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inafahamu ukubwa na umuhimu wa sherehe zilizotukabili za miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yatakayofanyika 12 Januari, 2014.

Miongoni mwa mambo makubwa yaliyotukabili kwenye uwanja wa Amaan ni Mashindano ya Kombe la Mapinduzi na gwaride siku ya kilele cha sherehe hizo. Kwa kufahamu hayo wizara imejiandaa vya kutosha kuufanyia matengenezo makubwa uwanja huo wa amani, ili kuweza kupatikana kwa huduma muhimu zikiwemo kurekebisha mfumo wa maji na kiwanja kukiwekea nyasi bandia, ili kuwa na hadhi inayolingana na sherehe hizo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa majibu ya Mhe. Waziri amesema kwamba wizara imejiandaa kufanyia ukarabati uwanja ule. Je, ni lini hasa kazi hiyo itaanza.

(b) Kwa kuwa ni miezi sita tu iliyobakia, kuna uhakika gani kwamba Januari 2014 uwanja ule utakuwa tayari kwa ajili ya sherehe za Mapinduzi ambayo inatimia miaka 50.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii, na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli wizara yangu imejiandaa vya kutosha na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nawaomba kwa heshima na taadhima kwa maelezo haya ya kina ambayo nimeyaeleza kwenye jibu langu mama ni kuwa mutuidhinishie fedha za bajeti, ili inapofika mwezi wa nane tuanze matengenezo ya Uwanja wa Amani na kuweza kufanikisha sherehe zetu za Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, siwezi kusema ni tarehe ngapi tutamaliza kuweka nyasi bandia. Kwa hivyo, kama tunavyojua kupanga ni kuchagua na kupanga wakati wowote ule unaweza ukaharibikiwa au ukafanikiwa. *(Makofi)*

Mhe. Salma Moh'd Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c).

Kwa kuwa Uwanja wa Gombani unategemewa kutumiwa kwa Sherehe za Mapinduzi na sherehe nyengine. Vile vile kwa kuwa Uwanja wa Amani umetengewa fedha kwa ajili ya matengenezo.

(a) Je, Mhe. Waziri wizara yake haikutenga fedha kwa ajili ya Uwanja wa Gombani.

(b) Ikiwa haikutenga ni kwa sababu zipi zilizopelekea zisitengwe.

(c) Ikiwa zimetengwa ni kiasi gani cha fedha zilizotengwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii, na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba hivi sasa tunasubiri bajeti yetu mutuidhinishie fedha pamoja na kuipitisha, ili tuweze kumalizia Uwanja wa Gombani. *(Makofi)*

Kwa kweli Mhe. Mwakilishi nafahamu kuwa ni mwanamichezo mahiri akiwa ni mwanamke nipo akaniuliza swali hilo. Kutokana na hali hiyo, napenda kumhakikishia tena Mhe. Mjumbe kupitia kwako Mhe. Spika, pamoja na kuwaomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi mutuidhinishie, ili tuweze kuufanyia matengenezo Uwanja wa Gombani kwa ajili ya kuweza kuburudika pamoja na kupata kucheza michezo kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Nam. 124

Malipo ya '*Night Call*' kwa Madaktari wa Pemba

Mhe. Rufai Said Rufai – Aliuliza:-

Kwa kuwa malipo ya wito wa daktari wakati wa usiku (*night call*) hufanywa kwa madaktari waliopo katika Hospitali Kuu za Zanzibar. Vile vile kwa kuwa Pemba ni sehemu ya Zanzibar na katika Hospitali tatu kuu za Mkoani, Chake Chake na Wete, madaktari huitwa kwa kazi za usiku. Pia kwa kuwa inasadikiwa kwamba madaktari hao hawalipwi '*night call*' wanapoitwa kufanya kazi.

Je, ni sababu gani za msingi zinapelekea kutolipwa kwa madaktari hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 124 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, madaktari wakiitwa usiku kufanya kazi hiyo kwa wao inakuwa ni kazi ya ziada na kesho yake asubuhi atatakiwa kwenda kazini kama kawaida. Vile vile kwa taratibu zilizopo inatakiwa kuwe na ratiba inayoeleza nani atakuwepo kazini na lini na aifuate. Siku alizopangiwa kazi ambayo ni *on call* anatakiwa mwisho wa mwezi alipwe.

Bajeti ya Wizara ya Afya ya posho hizo huwa zinapangwa tofauti kila kisiwa kinapanga zake kwa mujibu wa wafanyakazi wake, na wala sio kwamba zinatoka Unguja na kulipwa Pemba na hata idara kwa idara sehemu nyengine.

Kwa mfano, Hospitali ya Mnazi Mmoja inalipa wenyewe posho zao. Tatizo linalojitokeza ni kwamba posho ni sehemu ya *OC,* na kama mnavyofahamu *OC* upatikanaji wake. Kwa hiyo, zinalipwa zinapopatikana. Hata hivyo, kama kuna jambo zito na zinatakiwa fedha basi zinafanyiwa na posho inabidi

isubiri. Kutokana na hali hiyo, ndio maana unakuta wanaodai posho hufika miezi hata mitatu hawajapata kwa sababu ya usumbufu huo.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa Mhe. Naibu Waziri. lakini naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa madaktari hawa wa Hospitali za Makunduchi, Chake Chake, Kivunge, Wete, Mkoani na kadhalika, elimu zao zinalingana na hawa madaktari wa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Je, ni jambo gani linalosababisha hawa madaktari wa Hospitali ya Mnazi Moja kupata *night call* na hawa madaktari wa hospitali nyengine wasipate.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, madaktari walioko katika mahospitali hawako katika *level* moja ya elimu. Kwa mfano, kuna daktari *specialist*, madaktari wa kawaida, *Medical Assistance* pamoja na *MO* na hao kikada ni tofauti. Kwa hivyo, *on call allowance* zao pia zimepangwa kulingana na tofauti zao. Kwa maana hiyo, awe hospitali yoyote ile basi kiwango ndicho kitakachosema kulingana na kada ya yule mtu aliopo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, ahsante sana.

(a) Kama wizara imechukua hatua gani kuondoa tatizo hilo, kwa sababu limekuwa la muda mrefu na tukipiga kelele kuhusu *call*, na hata hivi jana Mhe. Spika hukuwepo, nilipiga kelele sana suala hilo, lakini leo karibu mwezi wa nne madaktari hawajapata *call allowance* zao.

(b) Kwa vile kilio chetu ni bajeti Mhe. Naibu Waziri uko tayari bajeti hii tuiondoe leo, ili tuirejeshe ikafanyiwe kazi kwa ajili ya kuongezwa fedha.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, hiyo si tusubiri kwenye majumuisho, kumbe maudhui yenyewe yako huko.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nasema hivi swali lako kwa kuwa umelitaja kwenye majumuisho kule michango, basi tusubiri wakati wa majumuisho litajibiwa vizuri. Mhe. Saleh Nassor Juma endelea.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya, naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba madaktari wanapewa *night call allowance* bila ya kujali hospitali aliyo, kama akaitwa kwenda kutoa matibabu, ukiachilia mbali kama yuko Mnazi Mmoja au Chake Chake, pia madaktari amewataja hapa kwamba akiwa na *MD.*

Lakini kwa sababu kwenye Hospitali za Kisiwa kile cha Pemba kwa mfano, Mkoani, Chake Chake na Wete, madaktari wananung'unika sana kwamba wao wanaitwa, yaani wanapata *night call*, lakini hawapati *night call allowance*, ingawa Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba *OC* hazitolewi. Mhe. Spika, wao ni karibu miaka mitano hawajapata *night call allowance*.

Je, Mhe. Naibu Waziri kama tutakuletea majina ya madaktari ambao wamefanya *night call* na bado hawajalipwa hizo posho zao. Kwa hivyo, yuko tayari kuendelea kuwalipa pamoja na kuwapa *arrears* zao za siku za nyuma kwa vile umekiri kwamba wanastahiki hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli anachokisema si uongo tunadaiwa sana *night call allowance* lakini huwa tunaziandika na tunajua kwamba hilo ni deni kwetu. Kwa kweli tatizo la Pemba kwamba hakuna madaktari wengi kama hivi walivyo katika hospitali nyengine, kwa sababu walioko kule wengi ni wageni ambao hiyo *allowance* hawa-*demand*.

Lakini waliopo pale ni wafanyakazi wengi wa kada nyengine ambao nao pia wanafanya kazi za ziada. Kwa hivyo, wale ukiwaweka katika *list* hawatakiwi kulipwa *on call allowance*, isipokuwa wanatakiwa kulipwa masaa ya ziada. Kwa mfano, ikiwa ni *nurse* anatakiwa alipwe masaa ya ziada na hilo pia tunalijua kwamba nalo ni tatizo. Sasa kinachotakiwa ni kwamba sisi tunaweka kumbukumbu kuwa tunajua hili linadaiwa.

Mhe. Spika, swali litabaki kule kule kwenye *OC*, kwa sababu hiyo si mishahara na *OC* zikipatikana, basi kidogo kidogo wanalipwa. Vile vile Pemba wanalo fungu lao kwa upande wa kila hospitali. Kwa mfano, Hospitali ya Mnazi Mmoja wanalo fungu lao, Kivunge wanalo fungu lao, sasa inategemea kile wanachokipata katika hospitali husika watakigawa vipi na kipi kifanyike mwanzo na hayo sasa inategemea na kile walichokipata. Lakini tunajua kwamba madeni yapo na *Inshaallah* tukipata fedha tutayalipa, hatukuwalipa leo basi tutawalipa kesho Kiama.

Nam. 51

Ujenzi wa Matangi ya Kuhifadhia Maji katika Shehia ya Mtambwe

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Katika Shehia ya Mtambwe Kaskazini na Mtambwe Kusini, kila shehia ina kisima kimoja cha maji chenye pampu ambazo zinafanya kazi za ziada katika kupeleka maji kwenye vijiji kadhaa ambavyo huduma hiyo ya maji imefika.

(a) Je, wizara ina mpango gani wa kujenga matangi ya kuhifadhia maji na kusambazwa sehemu zote husika, ili kupatikana urahisi wa pampu hizo kudumu muda mrefu.

(b) Kama wizara imejipangia mpango huo, ni lini utaanza kutekelezwa.

(c) Kiasi gani cha fedha zinazotarajiwa kutumika katika mpango huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Majina Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa Mtambwe ya Kusini kupitia Mradi wa Maji wa Daya kwa sasa mtandao haupo umeathiriwa na ujenzi wa barabara, na malengo ya Mamlaka ya Maji ni kusubiri ujenzi huo wa barabara ukamilike, ili mtandao huo ujengwe tena kama vile ulivyokuwa mwanzo.

Mhe. Spika, kwa sasa huwezi kufikiria ujenzi wa matangi wakati mtandao wa mabomba haujakamilika. Vile vile ikumbukwe kwamba mradi huu ulijengwa kwa mashirikiano ya nguvu za wananchi, *TASAF* pamoja na serikali, na kwa sasa mradi huu unaendelea na huduma vizuri bila ya tatizo lolote.

Kwa upande wa Mtambwe ya Kaskazini ni kwamba Mamlaka ya Maji kwa kushirikiana na wafadhili, wanao mpango wa kujenga mtandao wa mabomba katika vijiji vitatu; vijiji vyenyewe ni Kidundo, Chanjaani na Chekea na mfadhili ameahidi kutoa dola za Kimarekani elfu 60, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo wa mabomba na baadaye kuliangalia suala la ujenzi wa matangi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Kwanza nikubali kuwa ni kweli kuna ujenzi wa barabara, lakini kabla ya ujenzi huo wa barabara kulikuwa na mpango wa kujenga tangi hili mahala panapoitwa Miembe Mizizi na watu wa Mamlaka ya Maji walikuja kule na tukakubaliana. Kwa sababu hiyo ya makusudi

kabisa, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu ya Mawasiliano wakaonesha sehemu ya kupitisha mabomba mpaka hapo ambapo panataka kujengwa hayo matangi.

Mhe. Spika, mashine hizi au pampu hizi zinafanya kazi masaa 24 kwa kupeleka maji kwa mgao. Kuna vijiji bado havijapata maji na vinataka kupatiwa maji kama vile Chanjaani, Chekea pamoja na Kidundo kwa Kaskazini; na Makongeni, Tondooni, Mitambuuni na Kinazini kwa Mtambwe Kusini.

Barabara si sababu na tukichelewa kujenga matangi, pampu hizi zitakufa na zikifa ni hasara kubwa sana kwa serikali na tabu kubwa kwa wananchi, haoni Mheshimiwa upo umuhimu wa kwenda pamoja tukafanya *feasibility study* ya barabara inayojengwa na maelekezo waliyotoa miundombinu kabla ya kujengwa barabara ili tuwe na uamuzi mwengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji ina malengo makuu ya kuupeleka mradi katika vijiji hivyo vya Mtambwe, kama hivi vijiji nilivyovitaja. Lakini kinachotuzuia kwa sasa hivi ni ujenzi wa barabara, haiwezekani kabisa kupeleka miundombinu ya mabomba wakati kuna ujenzi wa barabara, na barabara ile hatujajua wapi inapokomea. Kwa hiyo tunachosubiri ni kwamba ujenzi wa barabara ule umalizike, tukisha tupeleke mitandao yetu ya mabomba ili wananchi hawa wa Mtambwe na wao wanufaike na huduma hiyo.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, Mhe. Waziri atanisamehe kwa kumpa taarifa ifuatayo ambayo haijui. Maji yanayopelekwa Kibundo ndio maji yatakayopelekwa Chekea na ndio maji yatakayopelekwa Chanjaani. Tumeshatafuta baadhi ya vifaa na tuna utaratibu wa kukata hiyo barabara kabla haijatiwa lami ili maji yapelekwe huko. Lakini swali langu mimi si kupeleka maji ni kujenga tangi kwa haya maji yanayopatikana kwa hivi vijiji yaweze kupatikana kwa kutumia matangi ili zile pampu zetu za visima viwili ziweze kupata uhai, zikiharibika kwa kufanya kazi masaa 24 ni hatari.

Kwa hivyo suala hili asiliingize kwa kupeleka maji, suala liliopo ni ujengaji wa tangi ambao utakusanya maji ya visima viwili kwa pamoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ni kweli katika Jimbo la Mtambwe linahitaji kujengwa tangi. Vile vile na sisi tunaangalia utaratibu wa ule mtandao wa mabomba vipi unavyofikia. Nimuahidi Mhe.

Mwakilishi asiwe na wasi wasi na suala hilo, kwa sababu kama nilivyojibu hapo awali kwamba ukimalizika mtandao wa mabomba basi tunaangalia ujenzi wa tangi. Kwa hivyo asiwe na wasi wasi na suala hilo.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika hapa katika hali ya afya na usalama. Kwa kuwa Mtambwe ilikuwa na matatizo makubwa sana ya maji. Na kwa kuwa tulifanya kazi kubwa sana ndio tukapata mtandao wa maji, niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia TASAF ambayo ndiyo iliyotuwezesha mradi huu kupata maji katika Mtambwe.

Je, Mhe. Waziri haoni kwamba sasa hivi anawasumbua wananchi kwa kutopata maji ya kuridhisha. Na kwa kuwa Mtambwe ni muinuko katika jiografia yake. Huyo mfadhili ataanza lini kujenga na kuhakikisha kwamba wananchi wa hizo sehemu za Chekea, Chanjaani pamoja na Daya wanapata maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwamba tumeshazungumza na mfadhili na tumekubaliana kwamba katuahidi kutupa dola za Kimarekani elfu sitini kwa ajili ya kufanyia shughuli hizo. Kwa hiyo Wizara yangu itaelekeza macho yake katika eneo hilo la Mtambwe na tutahakikisha kwamba baada ya kujenga huu mtandao wetu wa mabomba basi tutajenga tangi kwa ajili ya wananchi hao.

Vile vile nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa jitihada zake. Mimi mwenyewe nimetembelea kijiji hicho na nikaona jitihada zake, kuna baadhi ya vitongoji ambavyo vilikuwa maji hayajafika Mhe. Mwakilishi kachangia kuwapelekea mipira na vijiji hivyo sasa hivi afadhali wananchi wake wananufaika. Kwa hivyo nimshukuru sana na sisi Wizara tutajitahidi kufanikisha zaidi ili mtandao huo upatikane kwa uhakika.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake alipokuwa akijibu alisema anasubiri barabara imalizike ndivyo aweze kupeleka miundombinu ya maji. Kama tunavyoelewa barabara zinajengwa kwa gharama kubwa sana, hii yote ni mipango ya serikali kupeleka huduma kwa jamii. Haoni kusubiri barabara ikamalizwa kujengwa halafu yeye akaenda kuvunja ni kutumia vibaya pesa za serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwanza naomba ieleweke kwamba Mtambwe maji yapo na uko mtandao wa zamani ambao bado wananchi wa Mtambwe wanafaidika. Isipokuwa maji yaliyokuwepo hayatoshelezi kutokana na kwamba mtandao uliokuwepo ni wa kizamani na haupeleki huduma kama vile unavyotakiwa. Sasa huo mtandao ambao tunataka kuujenga tena ni *line* mpya ya maji. Ndio maana tukasema kwamba tunasubiri ujenzi wa barabara umalizike ili tujenge hiyo *line* mpya. Kujenga *line* mpya ina maana haitoathiri au haitotofautiana katika ujenzi wa barabara na ujenzi wa *line* mpya. Tunachosubiri ipite barabara kwanza ili tusiingiliane katika ujenzi wetu na ujenzi wa barabara.

Nam. 84

Upanuzi wa Barabara ya Chakechake - Mkoani

Mhe. Nassor Ali Salim - Aliuliza:-

Kwa kuwa barabara ya Chakechake - Mkoani imekuwa ikisababisha ajali za mara kwa mara kutokana na wembamba wa barabara hiyo hali inayopelekea wananchi wengi kupoteza maisha.

Je, Wizara haioni haja ya kuifanyia miundombinu mipya ya kuipanua barabara hiyo ili kupunguza ajali hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 84 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba ieleweke kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano hatuna takwimu sahihi juu ya ajali zinazotokana katika barabara ya Mkoani hadi Chakechake ambazo zimesababishwa na wembamba wa barabara. Aidha wembamba wa barabara hiyo haijawa sababu kuu inazopelekea ajali hizo za barabarani. Naomba ikumbukwe kwamba pamoja na wembamba huo bado alama muhimu za kuongoza matumizi ya barabara zimo katika barabara husika.

Serikali imeliona tatizo la wembamba wa barabara hiyo na hatua ya awali tunachokifanya ni marekebisho madogo madogo ikiwa ni pamoja na kuimarisha maeneo ya pembezoni mwa barabara, yaani kwenye mabega kwa kuanzia na sehemu ya Mtambile hadi kuja Chakechake, na baadae kumalizia sehemu iliyosalia kurudi eneo la Mkoani.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa barabara ya Mkoani - Chakechake ni barabara kubwa na ni muhimu kwa watu wa Chakechake - Mkoani pamoja na Pemba kwa jumla. Na kwa kuwa barabara ile inabeba magari makubwa yanayobeba shehena kubwa hasa ukizingatia kwamba kuna bandari inayoshusha mizigo ya kampuni mbali mbali zinazotengeza njia na mambo mengine pale Pemba.

Na kwa kuwa barabara ile hivi sasa imechimbika kutokana na ubovu wa barabara ile. Na kwa kuwa barabara ile imekabiliwa na kona au krosi nyingi. Je, wizara yako Mheshimiwa ina mpango gani wa kuijenga upya barabara ile na upunguzaji wa krosi zilizomo ili kuondoa ajali. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwamba barabara hii ni nyembamba kulingana na matumizi halisi yaliopo hivi sasa. Barabara hii ina upana wa mita 6, matarajio yetu kwamba tukiweza kuongeza mita moja kila upande ikifikia kiwango cha mita nane inaweza ikakidhi kupunguza msongamano ambao unafikiriwa kwamba ungetokezea. Yale maeneo ambayo yamekuwa na athari na dosari. Wizara yetu inaendelea kuyafanyia ukarabati na kuyaimarisha maeneo hayo. Naamini yeye mwenyewe Mhe. Mwakilishi kama amepita ataona jitihada tunazozichukua katika uwekaji wa viraka na kuimarisha barabara ya maeneo hayo.

Suala la barabara hii ina krosi na kona nyingi haya ni maumbile ya kisiwa cha Pemba kilivyo, tukihitaji kujenga barabara zilizonyooka gharama za ujenzi nazo zitakuwa mara dufu ni kubwa. Kama tunavyotambua pamoja na wembamba wa barabara ile tukihitaji kuongeza mapana kwa kiasi hicho tutahitajika kutafuta fedha nyingi kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wetu, kukata ardhi, kulipia miti na gharama nyengine.

Nimuombe Mhe. Mwakilishi, kwa muda huu serikalini hatuna mpango wa leo na kesho katika kujenga kwa mapana kuongeza barabara hiyo. Isipokuwa kwa kipindi cha muda mfupi tuna makusudio ya kuongeza upana wa mita mbili upande mmoja mita moja na upande wa pili mita moja ili kuweza kunusuru na kuimarisha miundombinu hiyo ya barabara ili kuweza kukidhi mahitaji na matumizi mazuri ya huduma ya barabara.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa barabara hiyo hivi sasa inakatwa katwa vipande katikati ya

barabara ambavyo, huita ni viraka na viraka vile vinasababisha ajali kwa waendesha baskeli, pikipiki na magari.

Je, Mhe. Waziri huoni ni aibu kwa barabara ile kuu kukatwa vipande kama vile ambavyo vinahatarisha maisha ya watu. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kama sote tunavyojua barabara kuu kutoka Mkoani kuja Chakechake ni moja haina sehemu ya kuweza kumruhusu mtu kuweza kutumia barabara ya pili. Kama barabara hii itakuwa ina tatizo tutahitaji barabara hiyo tuichimbe, tuikate tuweze kuweka kiraka. Kipindi hicho ambacho tunakata barabara hiyo tunaweka hicho kiraka watumiaji wetu wa barabara ni lazima wawe makini kuweza kunusuru. Ningependa pale tunapokata pawe na barabara nyengine ya kuweza kutoa huduma. Lakini kwa maumbile na unyonge wetu tumeshindwa kujenga barabara nyengine.

Nimuombe Mhe. Mwakilishi barabara yetu nyengine tukijenga itakayotoka Ole kwenda Kengeja inaweza ikawa manusura kwa kipindi kama hicho ambapo barabara itakuwa mbovu inawekwa kiraka kuweza kunusuru watu ambao hawafuati taratibu na masharti ya matumizi mazuri ya barabara. Alama za barabarani zinakuongoza kila barabara inapokatwa kunakuwa kuna alama zaidi ya mita mia moja kwamba mbele kuna kazi inaendelea, kwa hiyo unaelekezwa kwamba punguza mwendo, endesha chombo chako kwa tahadhari.

Naomba nichukue nafasi hii kutoa wito kwa madereva wetu wote wawe waangalifu na kuzingatia taratibu na sheria husika za kuongoza mwenendo wa matumizi mazuri ya barabara.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la mwisho la nyongeza.

Mhe. Spika, wakati barabara hii ya Mkoani - Chakechake ilivyokuwa inajengwa na kampuni ya PRIZIMO mimi nilikuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na wakati ule nilikuwa nikipinga moja kwa moja mia juu ya mia kuhusu ujenzi huu, lakini serikali ilikuwa ikikingia kifua. Sasa leo Mhe. Waziri anasema kuwa iko haja ya kuongeza mita moja huku na mita moja huku.

a) Je, serikali ilikuwa haioni kuwa kweli Kampuni ile ilikuwa haifai tokea wakati ule na ikaruhusu kujenga barabara ile nyembamba kwa sababu ilikuwa pesa ni kidogo au vipi.

b) Hivyo kuongeza mita moja upande huu na mita moja upande huu ili barabara iweze kupitika vizuri. Mheshimiwa amefanya utafiti na kuona eneo lote na krosi zile mita hizo mbili zitaweza kuongezeka huku na huku na wakati serikali haina fedha za kutosha kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, suala la awali la kuhusiana na kampuni za ujenzi wa barabara.

a) Naamini muda wa kulalamika kwenye hilo umeshapita. Sisi kama serikali tumejengewa barabara wakati wa kupima ni kipindi ambacho kimejengwa kabla ya kukabidhiwa kwetu. Baada ya kukabidhiwa kwetu hatuna nafasi tena ya kuweza kumlalamikia mjenzi wa barabara hiyo, yeye jukumu lake limeshakamilika.

b) Mhe. Spika, ni kweli tunaendelea na utafiti huo na kama nilivyojibu katika majibu yangu ya msingi nimeeleza kwamba matarajio yetu tunaanzia maeneo ya Mtohaliwa kuja Chakechake. Maeneo ambayo haya yanatupa ule muono kwa jinsi barabara pamoja na kuzingatia kona tutawezaje kuongeza hicho kipande cha mita moja kwa kila upande. Kwa kuanzia na hilo tumeanza barabara ya kutoka Chakechake kuelekea Machomanne pale, tunachukua kipande cha kilomita tatu, tumeshaanza kuweka mabega kwa njia ya kifusi, tukisha tunaanza kuweka lami. Baada ya kuona ufanisi wa huku tutarudi huku Mtohaliwa kuja Chakechake nayo kufanya hatua kama hiyo. Baadaye tutakuja Mtohaliwa kuelekea Mkoani, ili kuona kwamba ufanisi tumefanikiwa kwa kiasi gani. Lakini *pilot study* yetu tunaanzia Machomanne kuelekea Kwale kipande cha kilomita tatu tutaanza kuweka lami sasa hivi. Sasa kuona mafanikio yamefanikiwa kiasi gani katika uimarishaji wa uingizaji wa mabega ya barabara hizi ambazo tunazizungumzia.

Nam. 150

Vipi Serikali Imenufaika na Uwakala wa Meli za Kimataifa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu Nam. 150 naomba uniruhusu kusema machache. Kwanza nataka nimpongeze Dokta Mohammed Ali Shein kwa hotuba aliyoitoa jana Bandarini kuhusu wawekezaji wazalendo wa nchi hii kupewa nafasi ya mbele ya mwanzo. Nataka nimwambie Mhe.

Naibu Waziri awe tayari kuja kupokea Wawekezaji na asije akapiga chenga kama kawaida yake.

Vile vile kabla ya kujibiwa swali hili nataka nimpe pole lile swali lilokuwa lijibiwe hapo nyuma lakini inaonekana Naibu Waziri alikuwa hajajipanga, na leo hii nafikiri yupo tayari kujibu swali hilo. Mhe. Naibu Spika, naomba swali langu lijibiwe.

Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) imekuwa ikisajili Meli Dubai kupitia Kampuni ya Uwakala iliyofunga mkataba na serikali. Je, serikali imenufaika kwa kiwango gani cha mapato tangu kusajiliwa kwa meli za kigeni.

(a) Kwa mara ya mwisho Ukaguzi wa Ndani wa Hesabu ulifanyika kwa Kampuni hiyo nini matokeo ya ripoti yake.

(b) Chini ya mkataba Wazanzibari wanne (4) wanatakiwa kunufaika na ajira Jee, wangapi washanufaika na utaratibu huo.

(c) ZMA inaingiza fedha za kigeni kwa usajili wa meli kwani serikali imeshindwa kuwapatia 670 milioni za kuweza kununua vifaa vya mawasiliano na gharama za kutunga Kanuni za Sheria ya Mamlaka hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 150 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifutavyo:-

Mhe. Spika, lakini kabla sijamjibu naomba nimwambie Mhe. Jaku, kwamba sio kujipanga, nilikuwa ingawa Waziri wangu alikuwepo. Kama upangaji wa maswali sio jukumu letu siye wizara ni jukumu na usimamizi wa Baraza. Kwa hivyo mimi sikwenda kujipanga wala sikuja kwa ajili ya yeye, mimi nimekuja kutimiza wajibu wangu kwa niaba ya Serikali yetu.

Mhe. Spika, ni kweli Mamlaka ya Usafiri Baharini imekuwa ikisajili meli kupitia Kampuni ya Uwakala inayoitwa "*Philtex"* iliyoko Dubai na kufaidika kwa kiwango cha asilimia 65 kwa meli zinazosajiliwa na asilimia 35 inakwenda kwa Kampuni hiyo.

(a) Ukaguzi wa mahesabu mara ya mwisho ulifanyika kwa Kampuni hiyo kuanzia tarehe 21 Novemba, 2012 hadi 28 Novemba, 2012 katika Afisi zao zilioko Dubai na ulifanywa na Mkaguzi Mkuu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Tunapenda kukujuilisha

kuwa ripoti ya ukaguzi huo tayari imeshapelekwa serikalini kupitia wizara yetu, na hivi sasa inafanyiwa kazi.

(b) Mhe. Spika, tunapenda kulifahamisha Baraza lako Tukufu katika mkataba wa SMZ na *Philtex* hakuna Wazanzibari wanne walioainishwa kunufaika na mkataba huo, isipokuwa serikali kwa ujumla wake na *Philtex* kwa uapande wa pili.

(c) Ni kweli Mamlaka ya Usafiri Baharini inaingiza fedha za kigeni katika usajili wa meli za nje TZIRS *"Open Registry"* fedha hizo huingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali na Mamlaka huziomba fedha hizo kwa ajili ya shughuli mbali mbali za kiutawala na uendeshaji wa majukumu hayo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri ambayo hayakukidhi swali la msingi kama nilivyomuuliza.

a) Baada ya mkaguzi kukamilisha kazi yake ni kitu gani ambacho amekigundua katika ripoti yake na Zanzibar imenufaika na mapato kiasi gani tangu kufungwa kwa mkataba huo. Ripoti hiyo baada ya kutoka kwa mkaguzi lini italetwa Barazani.

b) Serikali imetumia vigezo gani kabla ya kufunga mkataba wa miaka kumi na Kampuni ya *Philtex.* Mkataba huo umeizuia serikali kuingia mkataba na kampuni nyengine zaidi ya hiyo kwa muda huo (*excuse*).

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa sana namuomba Mhe. Jaku azungumze taratibu niyapate yote ili niyajibu kwa ufasaha. Maana amekuwa na desturi kadri anavyojibiwa haridhiki, kwa hivyo namuomba tu azungumze taratibu niyapate yote nimjibu kwa ufasaha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika,

a) Baada ya mkaguzi kukamilisha kazi yake ni kitu gani ambacho amekigundua katika ripoti yake. Na Zanzibar imenufaika na mapato kiasi gani tangu kufungwa kwa mkataba huo. Na lini ripoti hiyo italetwa ukizingatia tokea kufungu kwa mkataba huo ilikuwa ni mwaka 2007/2008 mpaka leo 2012. Sijui umenielewa?

b) Serikali imetumia vigezo gani kabla ya kufunga mkataba wa miaka 10 na Kampuni ya *philtex*, mkataba huo ambao umezuia serikali

kuingia mkataba na kampuni nyengine zaidi ya hiyo kwa muda *(excuse).*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tumeeleza katika majibu ya msingi kwamba SMZ imeingia mkataba na *philtex* na sisi kama Wizara tumekwenda kufanya ukaguzi kwa kupitia wataalamu wetu. Utaratibu wa serikalini tumefanya uchunguzi, ripoti inakwenda serikalini kufanyiwa kazi kwa taratibu husika hasa wenzetu wa Wizara ya Fedha na wanaohusika. Baada ya hapo maelekezo ya serikali yote yatakayoelekezwa tutalijulisha Baraza hili Tukufu, lakini kumwambia lini tutaleta ripoti hiyo siwezi kutoa kauli hiyo.

Jambo la pili kiasi gani serikali imenufaika, tutamletea kwa maandishi kwa mujibu wa taratibu za fedha zinavyoruhusu.

Suala la pili la mkataba, Mhe. Spika, serikali imejiridhisha kwamba kwa wakati huo Mkataba huu umefungwa mwaka 2007 kama tunavyokumbuka kipindi hicho ndicho kipindi ambacho SMZ ilikuwa katika mchakato mkubwa wa usimamizi na uanzishaji wa *Zanzibar Maritime Transport Act* kwa kupitia msaada mkubwa walioupata Zanzibar kwa kupitia Shirika la IMO. Malumbano yalikuwa marefu kati ya serikali mbili hizi ndio SMZ wakaona ili kuimarisha chombo na utaratibu mzuri wa kuendesha shughuli za usafiri baharini, wakaona waingie mkataba na kampuni husika ya *philtex* kwa malengo ya kutaka kuona kwamba na sisi tunaanzisha taasisi ambayo inaweza ikajimudu na kujiendesha.

Kwa hivyo katika mkataba ule ni mkataba wa miaka 10, lakini tumepewa nafasi ya kila miaka mitano kuweza kuupitia na kuuhakiki upya pamoja na kuongeza matakwa na masharti ambayo yatakuwa yana tija kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kipindi hiki Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeunda Tume ya wataalamu inaupitia mkataba huo na tumefungua mazungumzo na wenzetu wa *philtex.* Matumaini yetu tutafikia pahali pazuri kwenye tija na serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na wananchi wetu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya mdogo wangu hapa Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) ni mamlaka ya Serikali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), na kwa kuwa katika usajili wa meli hizi mamlaka hii inapata fedha. Na kwa kuwa kazi yetu sisi Wawakilishi sio kuwapitishia bajeti zenu tu hapa serikali kama mnavyofanya

sasa, lakini kuangalia matumizi mazuri ya fedha za walipa kodi wa nchi hii zikiwemo hizo zinazopatikana baada ya usajili wa meli hii ukiachilia mahesabu ya mkaguzi wa ndani.

a) Je, kuna ukaguzi wowote uliofanywa na Kamati yetu inayoshughulika na mambo ya madukhuli humu Barazani ya PAC ishawahi kufanya ukaguzi wa fedha hizi.

b) Na kama haijawahi lini itakwenda ili wananchi wajue hasa ule mtiririko wa fedha unaoingia katika suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba fedha zote zinazoingia kupitia ZMA na chombo hichi cha *Philtex* matumizi yake ni mazuri sana, hakuna ubadhirifu wala hakuna upotevu. Nimuhakikishie Mheshimiwa Mwakilishi kwa kuwa fedha hizi zinaingia katika mfuko Mkuu wa Serikali, naamini kwamba chombo chetu cha Baraza la Wawakilishi yaani (*PAC*) itakuwa inakagua na kutoa ushirikiano unaostahiki. Sisi kama Wizara majukumu na wajibu wetu ni kufuata taratibu za fedha kwa mujibu wa muongozo wa serikali. Kinachoingia katika wizara hii kwa kupitia Shirika hili moja kwa moja kinakwenda katika mfuko Mkuu wa Hazina.

Kwa hivyo kama kutakuwa na muongozo wowote wa kuweza kuionesha *PAC* kwenda kukagua nje hatuna *objection* lakini tunaamini kwamba mfumo mzuri wa serikali ni kwamba fedha zinazotoka nje zikija zinakwenda moja kwa moja Hazina na *PAC* wana nafasi ya kwenda Hazina kwenda kufanya uchunguzi na kudadisi ili kuweza kujua matumizi na upatikanaji wa fedha hizi kwa msingi ule ule wa kuweza kuendeleza nchi yetu sote kwa umoja wetu.

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, mimi sijamwambia Mhe. Naibu Waziri kwamba fedha hizi hazitumiki vizuri, zinatumika vizuri kama wanavyotumia fedha zao jamaa zetu wa Wizara ya Afya hapa na wanakwenda PAC kutizama kule. Sasa mimi nadhani Mhe. Spika, katika hili uwepo utaratibu nadhani ingekuwa vyema na Kamati yao uliyoiunda ya *PAC* ikawa inapangiwa hasa kwenda kuangalia utaratibu na mtiririko wa fedha kwa hii Kampuni.

Mhe. Spika: Sasa maelekezo gani unataka.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Maelekezo ninayotaka ni kwamba uielekeze kamati yako kwenda pale sio una wasiwasi kwamba zinaibiwa fedha, lakini ni

utaratibu kwamba walipa kodi wajue mwenendo wa fedha za nchi. Kwa hivyo tunakuomba utuelekeze hapa Mheshimiwa.

Mhe. Spika: Maelekezo ya aina hiyo huwezi ukatoa hapa. Ameshajibu yeye anavyoona kama kuna jambo ambalo lina matatizo basi yule *CAG* anaweza kufanya kazi yake akaenda akaangalia na *PAC* ikafanya kazi yake.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini napenda nimuulize Mhe. Naibu Waziri. Pamoja na fedha nyingi zinazopatikana kwa ajili ya usajili wa hizo meli kwa kampuni hii iliopo Dubai, lakini mamlaka ya usafiri baharini ina matatizo makubwa ikiwemo majengo ya Ofisi, Ofisi wanayokaa ni Ofisi ya kukodi na ni finyu haitoshelezi. Ni lini serikali itaona haja ya kuwapatia hizo fedha ili wajenge Ofisi ya kutosha ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Na jee, kuendelea kukodi jengo ambalo ni finyu zaidi hatuoni kama tunawanyima kutekeleza kazi zao kwa ufanisi na wakati vyanzo vya kupatia fedha za kujengwa ofisi zipo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, suala la ukosefu wa Ofisi katika serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar uko katika taasisi nyingi na kama Mhe. Mwakilishi ataweza kuchanganua kwa haraka haraka tu atakuta taasisi nyingi hasa zinazojitegemea kama *ZMA* nyingi hazina Ofisi. Sisi wenyewe kama Wizara mpaka muda huu hatuna Ofisi. Sasa madhumuni ya kutaka kuwa na Ofisi ni mazuri, malengo ya kutaka kuwa na Ofisi mazuri, kikwazo kiko katika upatikanaji wa fedha. Fedha hizi ambazo tunazozizungumzia hapa zinazopatikana kwa *ZMA* wao wenyewe hawazipati zote na wala haziwatoshi katika shughuli muhimu za kuendesha shughuli zao ikiwa ni pamoja na usimamizi wa usalama wa usafiri wa watu wetu baharini.

Nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba sisi kama Wizara tutaendelea kulihimiza hilo na kama tutaweza kupata nyenzo zitakazoweza kutusaidia, hatuoni shida wala hatuoni sababu ya kuwazuia wenzetu hawa wasijenge Ofisi zao. Kwa kipindi hiki tunaamini utaratibu waliotumia kwa kukodi jengo ni utaratibu mzuri kwa sababu watapata sehemu ya kuweza kutulia na kuweza ku-*concentrate* katika uimarishaji wa huduma zao kwa wananchi wetu.

Kwa hivyo malengo ya kujenga ofisi yapo kinachotukwaza ni upatikanaji wa nyenzo hasa fedha katika utekelezaji wa jambo hilo kubwa na muhimu kwa Wizara yetu.

Mhe. Spika: Naomba tukumbuke tu kwamba tunakusudia kufanya majumuisho asubuhi hii kwa hoja hii ya Wizara ya Afya, tuna wachangiaji wawili wengine tayari walielekezwa na Mhe. Naibu Spika, aliyekuwa amekalia kiti kama wana maelezo watoe kwa maandishi.

Kwa hivyo tuna wachangiaji wawili halafu baadae tunaita timu ya Mawaziri ili kuanza kufanya majumuisho. Kwa maana hiyo basi niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tunapotoka kwa ajili ya kwenda kupata upepo kidogo wahakikishe wanarudi ili tuje tuendeleze kazi hii kwa wakati, maana wengine tukitoka inakuwa tunakwenda moja kwa moja.

Wachangiaji wetu kwanza nimuombe Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na baadae Mhe. Panya Ali Abdalla. Nimeambiwa wanahitaji dakika tano tano tu hao.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Afya. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake pamoja na watendaji wake wote kwa hotuba hii ambayo wameiwasilisha ambayo imefafanua kila aina ya mambo.

Mhe. Spika, mimi nianze na hospitali ya Kidongochekundu. Nataka ninukuu kidogo Mhe. Spika, kuanzia Julai 2012 hadi Machi 2013 jumla ya wagonjwa wa nje 4522 walipatiwa matibabu na 2314 ni wanaume na 2208 ni wanawake. Mhe. Spika, kabla sijaimaliza hii niseme kwamba hospitali hii inahitaji kuangaliwa kwa kina kwa sababu wagonjwa wa akili ni wagonjwa ambao hawawezi kujishughulikia wala hawawezi kumudu hali zao.

Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri akaliangalia suala la Kidongochekundu kwa wagonjwa wale ili kulipatia ufumbuzi, na pia inasemekana kwamba hospitali ile haina mtaalam wa maradhi yale, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri alifanyie uchunguzi au alifanyie jitihada ya kupatikana mtaalam pale ili kuweza kuwatibu watoto wetu ambao ni wagonjwa wa akili.

Mhe. Spika, nije katika Mfamasia Mkuu. Kwa vile Mhe. Spika, nimeweka mada zangu naomba nizisome kwa mara moja. Mhe. Spika, Ofisi ya

mfamasia, naishukuru Wizara Mhe. Spika, kukiri kwamba upatikanaji wa dawa haukidhi mahitaji. Naishukuru serikali kwa kulitambua hili, lakini pamoja na hilo Mhe. Spika, niseme kwamba serikali iliamua kwa makusudi kuwaruhusu wadau wake kufungua hospitali ili kuisaidia mzigo serikali. Lakini vile vile Mhe. Spika, wapo wadau ambao sasa hivi wanahitaji kufungua hospitali hizo ili kuisaidia serikali mzigo.

Lakini pamoja na hayo wafanyakazi hao au wadau hao waliofungua hospitali hizo wanashindwa na wataalamu wa kuendesha hospitali hizo kama vile Mfamasia mkuu. Kwa hivyo Mhe. Waziri niseme kwamba ni vyema tukatafuta wataalamu ili kuwapeleka katika hospitali hizo wakaisaidia serikali zaidi na vile vile kwa kuwa tunao watoto wetu ambao wamesoma skuli hapo Mbweni ambao wamemaliza Mhe. Spika, kwa nini Mhe. Waziri hawaajiri watoto wale ili wakapata ajira zao katika kuanzisha hospitali hizo.

Mhe. Spika, nije katika kitengo cha maradhi ya kuambukiza. Kwanza naipongeza Wizara ya Afya kutambua kuwa yapo maradhi ambayo hayaambukizi, kama yalivyoainishwa katika kifungu 211, lakini pamoja na serikali kupewa maelekezo kwamba wale ambao wameshapata maradhi kama hayo wafanye mazoezi ili warudishe afya zao. Lakini je, kuna wale ambao bado hawajapata maradhi kama haya Mhe. Waziri hawa unatwambia nini?

Mhe. Spika, nije katika hospitali ya Muembeladu. Mhe. Spika, naipongeza Wizara kwa kupata madaktari wa upasuaji katika hospitali ya Muembeladu. Mhe. Spika, niseme kwamba hili Mhe. Waziri alione ni faraja kubwa ambayo pia ni furaha kwa Wazanzibari wote ambao pale watatokewa na matatizo wanajua kwamba wapo madaktari wa kuweza kuwasaidia.

Lakini vile vile Mhe. Spika, nimwambie Mhe. Waziri hawa wataalamu tuliowapata wa upasuaji awaengeenge kwa sababu Mhe. Spika, sasa hivi madaktari wengi wanaokaa hapa huwa wanatutoroka na wanatukimbia, na sijui sababu gani ambazo wanatukimbia kwa haraka. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri hawa awaengeenge ili kuwaridhisha na wao wasiweze kutukimbia.

Mhe. Spika, nije katika bodi ya vipodozi. Bodi ya vipodozi Mhe. Spika, pamoja na Waziri kusema kwamba alifanya ukaguzi katika maduka ya madawa. Lakini nimwambie Mhe. Waziri kwamba katika maduka hayo ya madawa vimo vipodozi, vyakula na madawa mengine ambayo haya wananchi wale hawayaainishi kwamba sehemu hii inakaa dawa au vipodozi na sehemu hii inakuwa na vyakula. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri awahamasishe wale wanaouza vyakula na vipodozi katika maduka ili waweze kuainisha baina ya dawa na vipodozi kuondoa athari kwa walaji wa vyakula vile.

Mhe. Spika, nije katika uchunguzi wa maradhi ya ukimwi, Mhe. Spika, niseme kwamba unapokwenda pale hospitali unapochekiwa maradhi ya ukimwi huwa unaambiwa kwamba subiri majibu, lakini kwa aliyekuwa anao ukimwi huambiwa njoo baadae au njoo na mzee wako. Sasa niseme kwamba Mhe. Waziri hii ni dunia ya utandawazi, na hivi sasa tumetoka kwenye *analogue* tumeingia kwenye *digital*. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri pale mtu anapochunguzwa yale maradhi ni vyema mtu yule kumwambia kwamba una tatizo hili ili aweze kujipanga na aweze kwenda kujiunga na wenzake ili kuondosha usumbufu na roho iweze kutulia.

Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hiyo. Ahsante.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi ninashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza kabisa na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye aliyetujaalia tukafika hapa tukawa salama, pia nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri na watendaji wake wote kwa kazi ngumu nzito lakini Mwenyezi Mungu atawapa nguvu na afya waweze kufanya vizuri.

Mhe. Spika, nataka nianze mchango wangu katika ukurasa wa 5 ambao kuna Idara ya Kinga na Elimu ya Afya. Mheshimiwa Idara niseme ni muhimu na kama usemi wa kitaalamu unavyosema *kinga ni bora kuliko tiba*, Idara hii ikijikita hasa katika kufanya kazi zake vizuri basi tunaweza tukapunguza asilimia kubwa ya wagonjwa kwa kuzingatia elimu tunayoipata na tukaweza kuifanyia kazi basi ingekuwa na tija kwetu.

Mhe. Spika, niende kwenye ukurasa wa sita ambapo kuna kitengo cha kufuatilia mwenendo wa maradhi nacho kina jukumu la kuratibu na kufuatilia mwenendo wa maradhi. Mhe. Spika, mimi niendelee kusema kitengo hiki kina umuhimu mkubwa kwani elimu inayotolewa inatakiwa iwe endelevu na isiwe elimu ya muda mfupi. Kwa sababu hapa tunakumbana na maradhi mbali mbali ya mripuko. Sasa niseme elimu hii iendelee kwa sababu tunaelimisha zaidi ule wakati wa mripuko wenyewe unapotokea. Na tunaacha hizi siku za kawaida ambapo ndio tunatakiwa tujikinge kabla huo mripuko haujatufika.

Kwa hivyo mimi niombe elimu hii iendelee kutolewa; kwanza kwa sababu tukizingatia vyanzo vyetu vya maji haviko salama tumevivamia, kwa hivyo niiombe serikali iendelee sana kutoa elimu hii na hasa tukizingatia katika mazingira pia hatuko salama. Kwa hivyo elimu hii iendelee kutolewa isiwe kama maji labda tuyachemshe wakati wa mvua tu za masika. Vyanzo vyetu vya maji haviko salama tuendelee kuchemsha maji kwa usalama wa afya zetu, tuendelee kuyatunza mazingira kwa usalama wa afya zetu.

Mhe. Spika, pia Wizara hii ya Afya utaliona jina lake afya ni dogo lakini majukumu yake ni makubwa sana. Kwa sababu ili tuwe na afya bora basi maji pia tuyapate yaliyokuwa yako salama, vyakula tuvipate viko salama. Vipodozi hivyo vinatajwa hapa basi viwe viko salama. Sasa mimi niiombe serikali inapokuwa na mipango basi iweze kupanga vyema na kuwa na mkakati wa pamoja kuonekana wao wenyewe kwa wenyewe kati ya Wizara na Wizara wakihimizana kuhusu masuala haya.

Kwa sababu tukisema Wizara ya Afya ili ihakikishe wananchi wake wanapata afya na kupunguza mrundikano wa kwenda mahospitali kwa wingi, basi ni lazima pengine Wizara nyengine ama ya biashara nayo iweze kufanya vizuri kuhakikisha vyakula vinavyoletwa vina usalama kwa wananchi ili tupunguze ule mrundikano wa kuiongezea mzigo Wizara ya Afya kutibu wananchi kila wakati. Lakini pia Wizara ya Maji tuhakikishe nako vyanzo vile vya maji vinatunzwa na vinakuwa salama hilo lote ni jukumu la Wizara ya Afya, maana inataka wananchi wake wawe katika afya bora ili wapunguze mrundikano wa kwenda kule na kuiongezea mzigo Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 9 ambako kuna kitengo hiki cha kupambana na maradhi yasiyopewa kipaumbele. Mheshimiwa kweli maradhi haya hayapewi kipaumbele lakini mimi niiombe serikali iko sababu pia ya kuyapa kipaumbele, kwa sababu tunayadharau lakini hatimae yanadhoofisha watu, tunaona minyoo labda unaweza ukasema ni maradhi ya kudharau lakini inaweza ikamsababishia mtu madhara makubwa na hata kupoteza maisha!

Mhe. Spika, mimi niseme labda serikali ijikite katika mpango ambao ulikuwepo zamani. Mimi nakumbuka zamani ukifika tu hospitali jambo la mwanzo ukimpeleka mtoto ulikuwa unaambiwa umeleta choo, kwa hivyo pale ilikuwa inajulikana maradhi ya mgonjwa haraka sana, lakini ukiacha utaratibu wa hivi sasa ukienda hospitali utaulizwa, una homa, unakohoa, unatapika, unaharisha, baada ya hapo utaandikiwa dawa utarudi. Kumbe yule mgonjwa pengine alikuwa ndio ana minyoo angeweza kupatiwa tiba kwa wakati ule na tatizo lingeondoka. Mimi naomba utaratibu ule wa kupima vyoo mara kwa mara hasa kwa watoto tukizingatia wanapata matatizo haya mara kwa mara. Niiombe serikali bado iendelee na utaratibu ule wa kuchunguza kwanza kuliko kuendelea kutibu, kuendelea kutibu, kumbe tatizo linachukua muda.

Mhe. Spika, niende ukurasa wa 11ambako kuna kitengo kile cha afya cha bandari au katika viwanja vyetu vya ndege. Wenzangu walisema lakini na mimi hili nalikazia kwa sababu pale kama tutafanya uzembe tunaweza tukasababisha madhara makubwa katika nchi. Anaweza kuingia mgonjwa anatoka nchi jirani huko sisi hatuna vifaa vyovyote pale ambapo tunaweza

tukamkinga mgonjwa yule tunaacha tu anaingia. Tumepita katika utembezi kwa sababu hapa Unguja hatujatembea sisi tukaviangalia hivi vitengo, lakini Pemba tulifika *airport* tukakikuta kile kitengo cha pale yupo tu muhusika lakini hana kifaa hata ile *panadol* hana. Sasa hili ni tatizo tunaweza tukasababisha madhara makubwa.

Mheshimiwa niende katika ukurasa wa 21 ambapo kuna hospitali hizi za vijiji *cottage hospitals.* Naishukuru Serikali na naipongeza kwa juhudi pamoja tunakuwa tunaona bado kwa sababu mahitaji tunayoyataka ni makubwa na bado tunapata madogo tunakuwa tunalalamika lakini kwa pale tunapopata mimi nataka kushukuru. Mmejitahidi hospitali hii ya Kivunge kuweza kuweka huduma zile za haraka haraka zinatusaidia, lakini pia niombe katika hospitali hii ya Kivunge katika wodi ya watoto pana karo pale liko vibaya sana na linatoa harufu kubwa sana, hili tuweze kulishughulikia ili watu wetu waweze kubaki katika hali salama.

Lakini pia mimi niseme tujikite sana katika hospitali hizi za vijiji, tukijikita kupeleka huduma katika hospitali za vijiji maana yake ndio tumeweza sasa kuipatia mwanya hospitali ile ya rufaa tunayoitaka iwe ya rufaa basi inaweza ikawa ya rufaa. Kwa sababu tayari itakuwa imepunguza ule msongamano ambao unatupeleka sisi kule mjini. Tukitengeneza vizuri hospitali zetu hizi za Wilaya maana yake tayari tutaweza kuipa mwanya sasa hospitali ile kubwa ya rufaa ambayo tunaitaka iwe ya rufaa. Kwa hivyo mimi naomba hizi huduma basi tukite sana katika hospitali hizi za vijiji ili kuwapunguza hawa wasije huku mjini.

Mheshimiwa niende katika hii huduma ya uzazi wa kinamama. Mheshimiwa huduma hii nakumbuka tulipata *offer* kutoka kwa Mhe. Rais, kinamama waweze kujifungua bila ya kudaiwa chochote. Lakini bado inaonekana katika huduma hii kuna malalamiko mengi, bado watu wanaendelea kudaiwa wachangie huduma hizi. Mheshimiwa hili naomba ulifuatilie kwa sababu kauli ikitoka kwa Rais huwa ni kauli kubwa, lifuatilie ili tuone wananchi wetu bado wanabaki katika kupata huduma.

Mhe. Spika, mimi naomba nimuombe Mhe. Waziri kuna wagonjwa hawa wa uti wa mgongo ambao wanakuwa hawajiwezi, miili yao imeregea kabisa na hasa niseme wale walioko kisiwani ambao wanahitaji kuletwa matibabu huku Unguja. Nimuombe Mhe. Waziri basi aweze angalau kupanga mwezi mara moja kuwapelekea madaktari, kwa sababu inakuwa ni usumbufu kuwabeba wagonjwa wale kuwaleta huku angalau tungeweza kuwapunguzia kuwapelekea madaktari japo mwezi mara moja wakaweza kupatiwa huduma kule kule.

Lakini jengine nimalizie Mhe. Spika, kwa kuipongeza sana serikali kwa kuweka huu mpango wa damu salama. Na nataka nichukue fursa hii kuwashukuru wale ambao wanashughulikia kitengo kile ambao wanahangaika huku na huku kutafuta damu ili kunusuru maisha ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, nichukue basi fursa hii kutoa wito kwa wananchi wetu kuweza kuwapa mashirikiano ya kutosha wenzetu hawa wanapopita katika kutafuta damu ili kuweza kuokoa ndugu na jamaa zetu. Kwa hivyo tujitahidi na tuungane nao na tuweze kuchangia damu bila ya matatizo yoyote ili tuhakikishe tunapata huduma bila ya matatizo. Kwa sababu kitengo hiki tangu kimeanza naona imekuwa tunakwenda vizuri hakuna mgonjwa ambaye anaweza kukaa akawa hajapatiwa damu kama ilivyokuwa utaratibu wa huko nyuma.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi naitakia kheri na fanaka Wizara hii iweze kupitishwa bajeti yake ili wananchi tuendelee kuwa na afya bora, kwa sababu kama hatukupitisha hapa basi inawezekana wagonjwa wengi tukawakosa na wengine tumesema hapa sote ni wagonjwa.

Baada ya kusema hayo kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100.

Mhe. Spika: Mhe. Fatma nikuombe radhi kidogo kuna Mhe. Mjumbe mmoja aliniomba dakika 5 tu ambaye ni Mhe. Salma Mussa Bilali na baada ya hapo nikuombe wewe sasa uchangie.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kukubali ombi langu na mimi la kunipa nafasi hii ya kuchangia angalau dakika 5. Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia salama na leo hii kuweza kuichangia Wizara hii.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar Dr. Ali Mohammed Shein kwa uamuzi wake wa kumteua Waziri na Mhe. Naibu Waziri na baadae kuwapa Wizara hii yenye umuhimu wa pekee, Wizara inayogusa maisha ya watu, wananchi pamoja na sisi viongozi tuliokuwemo humu, hivyo basi Mhe. Spika, nitoe pongezi zangu maalum kwa safu ya usimamizi iliyojipanga vyema kusimamia utendaji wa shughuli mbali mbali za sekta ya afya, chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja naWakurugenzi wake. Mhe. Spika, naomba niwashukuru sana.

Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza watendaji wote na watoa huduma ya afya kwa juhudi zao wanazozichukua kwa wananchi pamoja na

hali ngumu zinazowakabili. Mhe. Spika, pia napenda nipongeze juhudi za makusudi za Wizara ya Afya kwa uimarishaji wao wa huduma za afya katika ngazi ya vijiji na Wilaya, huduma ambazo zimepelekea kuweka uongozi maalum wa Wilaya, kuweka timu Unguja na Pemba, timu ambazo zinafanya kazi vizuri katika usimamizi wake na zinatoa vyema huduma katika vijiji mbali mbali.

Mhe. Spika, katika mchango wangu naomba nichangie katika ukurasa wa 21. Mhe. Spika, Mhe. Waziri hapa katika uwasilishaji wake alieleza kwamba hospitali ya Makunduchi imeboreshwa katika huduma mbali mbali za wananchi kama za upasuaji na mambo mengine. Lakini Mhe. Spika, nataka nimueleze kwamba wananchi wa Makunduchi wana malalamiko makubwa, pamoja na juhudi hizo ambazo zimechukuliwa lakini bado wana malalamiko wakubwa kuhusu daktari wa kuhudumia wananchi wa kawaida katika hospitali hiyo. Wamekuwa wakilalamika kwamba wanapokuwa na matatizo ya kiafya wanashinda kutwa hospitali, daktari mmoja anakuwa anahitajika katika sehemu, kwa hivyo wanakosa huduma na wanashinda pale wanaomba kwamba wapatiwe daktari ili aweze kutoa huduma kwa wakati.

Mhe. Spika, kwa hivyo naomba Mhe. Waziri atapokuja hapa anieleze ana mpango gani wa kuongeza madaktari katika hospitali ya Makunduchi ili aweze kuwaondolea matatizo wananchi wa Makunduchi.

Mhe. Spika, pia katika uimarishaji wa huduma za afya vijijini ni suala la msingi sana na suala hilo hata Mhe. Rais wa Zanzibar alipokuwa akitembelea katika ziara zake za Mikoa alilitilia mkazo suala hilo. Na Mhe. Rais aliomba kwamba Wizara ya Afya iweze kusukuma mbele nguvu za wananchi ambao wameanzisha majengo katika maeneo yao. Mhe. Spika, Mhe. Rais alitoa ombi hilo kwa Wizara ya Afya lakini Mhe. Waziri nilikuwa nataka atakapokuja hapa aniambie kwamba ni majengo mangapi au majengo gani ambayo tayari wameshaanza kutekeleza na kusaidia nguvu za wananchi.

Mhe. Spika, mimi nina mfano hai katika Mkoa wangu katika kijiji cha Mpapa. Kijiji cha Mpapa Mhe. Spika, kuna hospitali imejengwa siku nyingi kwa nguvu za wananchi na hivi sasa imeshafikia asilimia 60 ya umalizikaji wake. Lakini Mhe. Spika, mpaka leo hii bado Wizara haijachukua juhudi za kumaliza jengo hilo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja pia aniambie ana mpango gani wa kuweza kulimaliza jengo hilo. Kwa sababu jengo hilo litakapomalizika litawaondoshea shida wananchi wa vitongoji mbali mbali ambavyo vimezunguka katika kijiji cha Mpapa wananchi ambao wanaweza wakafika hata wananchi 20,000 kikiwemo kijiji cha Mpapa na vitongoji vyake

kama vile Pagali, Matora, Kivuzu, Vilima Viwili, Mgeni Haji na maeneo mbali mbali ambayo yanazunguka kijiji hicho. Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba atakapokuja anieleze Wizara ina mpango gani katika kuvimalizia vituo hivi.

Mhe. Spika, pia naomba katika Mkoa wangu huu wa Kusini kuna kituo cha Afya cha Unguja Ukuu, kituo ambacho kiko katika hali mbaya na kila siku tunasikia kiko katika mpango wa kumalizia lakini naomba Mhe. Spika, pia anipe maelezo kuhusu kituo hicho. Pia na kituo cha Umbuji ambacho imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wa Umbuji, maneno mengi, wameshalizungumza, na ahadi nyingi zimeshatolewa, lakini mimi nataka Mhe. Waziri, atakapokuja hapa aniambie ni lini wananchi wa Umbuji watejengewa kituo hicho, kituo ambacho ni kibovu, hakifai, wakati wa mvua wanashindwa kukaa katika kituo hiki. Naomba Mhe. Spika, Mhe. Waziri, aniambie ni juhudi gani zimechukuliwa au ana mpango gani wa kukimalizia kituo hicho cha Umbuji.

Mhe. Spika, naomba niipongeze Wizara ya Afya kwa dhati kabisa kwa kuandaa huu mfumo wa kuweka kumbukumbu za wagonjwa wa kitaalamu. Kwa sababu Mhe. Spika, kitengo hiki kilikuwa kinaweka kumbukumbu za wagonjwa kwenye mafaili, lakini mafaili hayo mgonjwa anapokwenda anakuwa anaambiwa *file* halionekani, lakini kwa kuwa wameanza kuweka mfumo huu wa *electronic* naomba niwashukuru sana kwa dhati na waendelee, ili mgonjwa anapokwenda akitaka kumbukumbu zake zipatikane kwa ufanisi.

Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa muda huo nina mengi kidogo lakini nashukuru kwa kunipa angalau muda huo kwa leo. Kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi naomba nianze kwa kumshukuru Allah kwa kutuamsha tukiwa wazima wa afya na kutukutanisha hapa tena kwa ajili ya kuendelea na shughuli hizi kwa manufaa ya wananchi wetu na nchi yetu kwa ujumla. Lakini nakushukuru wewe vile vile kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia machache kuhusiana na bajeti hii ya Wizara ya Afya.

Mhe. Spika, naanza kwa kumpongeza kwa dhati sana Mhe. Waziri wa Afya, Mhe. Juma Duni Haji, lakini na Naibu Waziri wa Afya, Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya, Jopo la Watendaji wote wa Wizara ya Afya, wakiongozwa na Katibu Mkuu wao Dkt. Mohammed Jiddawi, kwa maandalizi mazuri na hatimae kuweza kuwasilisha kitabu hiki cha bajeti chenye taarifa na takwimu ambazo zinaonekana kukamilisha kitabu hiki, na kukipamba zaidi kwa picha ambazo kwa kweli ukizitizama zinakupa mategemeo mema sana,

kukufurahisha kwenye moyo wako kwamba tunakokwendea katika suala zima la sekta ya afya katika kuimarisha vituo na hospitali zetu basi ni kuzuri sana, picha ambayo ipo katika ukurasa wa nyuma.

Mhe. Spika, nimesimama hapa kwa kuchangia suala ambalo mchangiaji mmoja jana alichangia kuhusiana na suala zima la kuondoshwa kwa unga mbovu ambao ulikuwepo Bandarini na akahitaji kusema kwamba unga huu uondoshwe ili usituletee madhara. Mimi nakubaliana nae na nimesimama kwa sababu suala hili liligusa taasisi nyingi sana hapa, lakini zaidi lilianza na Wizara ya Afya kupitia Bodi yao ya Chakula, Dawa na Vipodozi kwa kuweza kuukataa unga ule ambao kama tani 780 ulioletwa kwa ajili ya matumizi kwamba haufai kwa matumizi ya binaadamu, niwapongeze sana kwanza kwa umahiri na kuwa makini sana katika kulinda afya za wananchi wetu.

Mhe. Spika, baadae likaja tatizo ya jinsi gani unga huu utaondoshwa. Lakini nina furaha kusema kwamba kwa mashirikiano na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Mazingira suala hili tunalipatia ufumbuzi ambao kwa imani yetu ni mzuri ambao hautaleta madhara kwa binaadamu wala kwa mazingira yetu hapa Tanzania.

Mhe. Spika, tatizo kubwa tulilokuwa nalo ni jinsi gani unga ule tungeweza kuuharibu, yaani njia ya kuweza kuuharibu na wengi wa wataalamu walikuwa wanatupa fikra kwamba ungeweza ukasambazwa katika ardhi halafu ukafunikwa na udongo mwengine na baadae ukatiwa dawa kama *fumigation*, lakini kikwazo tulichokuwa nacho Zanzibar ni kwamba hata hilo eneo lenyewe ambalo lingeweza kumwagwa unga huo na kutawanywa basi tulikuwa hatuna.

Sasa tulifanya mashirikiano yetu kama kawaida na wenzetu wametusaidia, tumekaa kikao cha pamoja cha Mawaziri watatu, Waziri wa Afya, Waziri wa Mazingira kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano na mimi nikiwa na sekta hiyo ya mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kamati iliundwa na kikao hicho kilikaa tarehe 14 Mei, na kwa kuona umuhimu na athari ambayo ingeweza kutokea ilifika hadi tukaweka *deadline* kwamba basi ikifika tarehe 15 Juni unga huu lazima uwe umeondoshwa, na uko kwenye *process* ya kuharibiwa na ikiwezekana kuharibiwa kwenyewe kuwe kumekamilika.

Mhe. Spika, nashukuru kwamba kamati ile iliyoundwa ikiwa na wadau wa pande zote mbili; Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar na kutoka vitengo mbali mbali ikiwemo Bandari, Nemc, Bodi ya Chakula na Vipodozi ya Zanzibar, lakini vile vile Mamlaka ya Dawa na Chakula iliyopo kule Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini na wote ambao wangeweza

kuhusika katika suala lile kuanzia kuweza kuondoa unga ule mpaka uharibiwe walishirikishwa, na kamati hiyo iliyoongozwa na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, nina furaha kusema imefanya kazi nzuri sana na bila ya kuchelewa, kwa sababu walipanga ratiba yao na waliweza kuitekeleza uzuri sana.

Mhe. Spika, tarehe 1 Juni ilifanya *fumigation* ya unga huo katika Bandari yetu ambao ulikuwa kwenye Ma-*container* 30 na tarehe 8 Juni Ma-*container* hayo yote yalisafirishwa kuelekea Dar es Salaam na tumebahatika kwamba baada ya majadiliano katika kamati kumejitokeza njia ambayo si ya kuumwaga katika maeneo na kuufanyia *fumigation* lakini *Twiga Cement Factory* kilikubali kuingia katika makubaliano na Nemc ili kusaidia kuuharibu unga huo kwa kutumia *incinerator* ambayo wao wanayo, wanauchoma ndani ya kiwanda chao, na hadi kufikia tarehe 3 Julai basi tayari ma-*container* kumi na tano yameshaharibiwa ya unga huo na kazi hii inaendelea na bila ya kuwa na athari katika mazingira yetu au athari kwa jamii.

Kwa hiyo Mhe. Spika, nimesimama hapa kumueleza ndugu yetu ambaye amechangia nafikiri alikuwa Mhe. Mshimba, kwamba tatizo hili sasa limeondoka tumelipatia ufumbuzi wa kudumu. Na nitoe wito tu kwa wafanyabiashara wetu na wananchi kwa ujumla kuweza kuhakikisha kwamba bidhaa ikiwemo chakula na vifaa ambavyo vinaletwa ndani ya nchi yetu tuhakikishe kwamba viko katika hali ya usalama, hasa kwa sababu ikitokea tatizo la kuweza kuviharibu vitu hivi Zanzibar kama Zanzibar hatuna maeneo ya kufanya shughuli hiyo, yaani inabidi upate eneo kubwa uweze kuufanya na kuufanyia *fumigation*, haidhuru pia baadae kunaweza kuwa na athari kwamba mvua inaweza ikanyesha na maji yale yanaweza kuingia katika vianzio vya maji.

Mhe. Spika, wito wangu kwa jamii naomba sana tushirikiane kwamba kuhakikisha bidhaa wanazoingiza katika visiwa vyetu ziko salama kwa mazingira, lakini vile vile muhimu zaidi kwamba ziko salama kwa afya za wananchi wetu. Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ahsante Mhe. Spika, na mimi ninakushukuru sana kunipa wasaa mdogo kuchangia hotuba ya Makadirio ya Fedha kwa mwaka 2013/14 ya Waziri wa Afya Zanzibar. Awali ya yote naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100, na nawaomba Waheshimiwa wenzangu wote tuiunge mkono ili tumpe fedha aweze kuimarisha afya zetu na watoto wetu kwa jumla wote pamoja na vizazi vyetu.

Mhe. Spika, kulikuwa na hoja nzito sana ya kutaka kauli ya Serikali juu ya nia ya Serikali katika suala zima la sekta ya Afya, nafikiri hili ni suala lazima tulitolee kauli nzito kwamba Serikali imeshasema na inaendelea kusema wakati wote moja ya kipaumbele chake ni sekta ya afya, kuimarisha sekta ya afya na naomba ninukuu hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, wakati akiwasilisha mpango wa maendeleo wa makadirio ya mapato na matumizi, kama tunayo hapo naomba tuangalie ukurasa wa 28 Mhe. Waziri alieleza wazi wazi naomba dakika moja Mhe. Spika, niweze kusoma tupate ile mantiki yenyewe.

"Mhe. Spika, haitarajiwi kwamba vipaumbele vya Serikali viwe vinabadilika sana mwaka hadi mwaka, mengi ya maeneo ya kipaumbele yanahitaji uwekezaji wa muda mrefu ili kufikia malengo ya maendeleo ya nchi, tunahitaji kujenga taifa lenye maendeleo makubwa ya kiuchumi, lenye watu walioelimika, wataalamu wenye hadhi ya kimataifa na wenye siha na wasiosumbuliwa na maradhi yasiyoepukika".

Mhe. Spika, hiyo ni kauli nzito ya Serikali imeweka wazi kabisa muelekeo wetu kwenye upande wa sekta ya afya. Mhe. Waziri wa Fedha kaendelea.

"kwa kuzingatia ukweli huu bado kipaumbele cha Serikali kitaendelea kuwa katika kukuza kwa kasi zaidi uchumi wetu na kuongeza ajira hususan kwa vijana, kuimarisha ubora wa elimu, kuimarisha huduma za afya hususan katika upatikanaji wa dawa za lazima na katika upatikanaji wa maji safi na salama".

Mhe. Spika, hii ni hotuba ya Serikali na natarajia kama hotuba ya Serikali hivyo ni vipaumbele vya Serikali vimewekwa. Lakini Mhe. Spika, zaidi ya hayo hata ukifungua vile vitabu viwili ambavyo vimeambatana na hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha; kitabu cha kwanza na kitabu cha pili ukiziangalia sekta za afya zimeelezwa kwa makini kabisa na malengo yake ambayo tunayatarajia kwa mwaka ujao wa fedha. Lakini zuri zaidi katika huo mpango mpya wa rasimu ya bajeti inayotumia programu PBB kwa mwaka ujao wa fedha, sekta ya afya ni sekta moja wapo iliyopewa kipaumbele na naomba niseme kwenye utangulizi wake tu ukurasa wa kwanza, anasema kwamba:

"Kama ilivyoelezwa katika matoleo mbali mbali ya Serikali mageuzi ya bajeti yanayotumia programu maalum yaani *program based budget* yatapelekea ufanisi katika changamoto zinazoikabili bajeti ya Serikali kwa sasa, na inategemewa kwamba yataleta uwiano mzuri wa sera za kisekta na kitaifa kwa jumla".

Mhe.Spika, hizo programu zenyewe zimewekwa katika kiambatanisho tulichopewa na wameonesha hasa bajeti ambayo imewekwa kwa mwaka ujao wa fedha. Sasa hili Mhe. Spika, nimeomba nilitolee ufafanuzi mdogo tu kuonesha nia ya Serikali na mtizamo wetu na muelekeo wetu kwenye sekta ya afya. Tunaposema kwamba Serikali haiko *serious* katika sekta ya afya si kweli hata kidogo, na kwa kweli Serikali imejidhatiti kwa upande wake wa fedha zake, lakini hata kutafuta wafadhili au wahisani na tunawashukuru sana wahisani wetu wametuunga mkono sana Mheshimiwa.

Mhe. Spika, tukiangalia hili buku letu la bajeti la vifungu buku kubwa hili, kitabu cha pili Vol.II, ukiliangalia kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ukurasa wa 465. Ile Idara ya Sera, Mipango na Utafiti imewekwa ile miradi ya maendeleo, miradi ya maendeleo kwa jumla niliyoipata mimi iko kumi na moja. Katika hii kumi na moja Mhe. Spika, minane ina pesa za SMZ na ina pesa za *grant* sio mkopo, *grant* hiyo nafikiri tutafautishe *grant*, hizi fedha za wahisani wetu na hizi Mhe. Spika, tuwashukuru sana wataalamu wetu ni utundu wao, uwajibikaji wao wanavyohangaika kuzitafuta pesa hizi za *grant* kwa sababu sekta ya afya *alhamdulillah* ni sekta kubwa sana lakini ina ushirikiano mkubwa sana *globally* huko WHO, UNDP.

Sasa unategemea ule utundu wako wa kuhangaika. Sasa tuwapongezeni sana Wizara ya Afya jamani kwa kweli kazi wanaifanya kutafuta msaada. Wewe ukiangalia ukurasa niliosema ule 465 utaona hiyo miradi ina *grant* halafu ina pesa zetu za SMZ. Kuna mradi mmoja ndio wenye *loan* na una pesa za SMZ, lakini kuna miwili haina *grant* wala *loan* ina pesa tu za SMZ.

Mhe. Spika, lazima tukumbuke mchango wetu takriban siku zote ni mdogo siikumbuki *ratio* gani tunatakiwa tuchangie labda mwenyewe Waziri wa Fedha na Naibu Waziri, watazungumza, lakini kuna kiwango fulani ambacho sisi lazima tutie ili na hizi fedha za nje tuzipate. Sasa hiyo tumeonesha *commitment* kubwa sana kwa upande wetu na Mhe. Spika, hata ukiangalia hivyo vifungu utaviona vilivyotuna mwaka huu kwa makusudi vimetunishwa ili mfano fedha za DANIDA za kwenye dawa akiondoka tuweze kujitegemea wenyewe, hayo ndio madhumuni.

Kwa hiyo Mhe. Spika, mimi naomba kusisitiza tu kwamba kwa kweli katika moja ya sekta ambazo Serikali imejidhatiti kulishughulikia ipasavyo ni sekta ya afya. Mhe. Spika, ulitupeleka Uchina tukasome sio maendeleo ya mageuzi ya kiuchumi tu hata mageuzi yao ya kiafya, na walituambia wakati wanakwenda katika mageuzi yote ya jumla ya nchi yao, moja waliyoipa kipaumbele ni mageuzi ya sekta ya afya, wakafundisha watu wao wote, madaktari wakapeleka ulimwengu mzima, wakafungua *academy* za afya,

yaani wameiendeleza sekta ya afya kama sekta nyengine, ndio maana leo unaona Wachina wanajitegemea wenyewe na wanatusaidia sisi wengine.

Hivyo mimi ninataka nisisitize hilo tu kwamba takriban tumejitahidi na hiyo ni dhamira yetu pesa nyingi sana tumepata tumeziwekeza kwenye afya na tumenunua vitu vingi tu, kwa hiyo tunaposema Serikali haishughulikii si kweli kabisa, hiyo ni nia yetu imekuwepo na itaendelea kuwepo, na hata kama uwezo wetu mdogo hapa tunasema tuwapeleke nje, Serikali inatumia fedha za kigeni kupeleka raia wake nje kutibiwa, kwa sababu uwezo hatuna hiyo tukubali.

Mhe. Spika, sasa ndio tunasema kwamba hiyo miundo yetu tuiimarishe, kwa hiyo nimesema nisisitize, halafu nimalizie kwa dogo tu ambalo nalo limezungumzwa na baadhi ya Wajumbe, wameonesha kama kuna ubaguzi kati ya pesa zinazopelekwa Pemba kwamba ni kidogo na pesa za Unguja ni nyingi, hilo sio lengo la Serikali hata kidogo, ninachoomba sana tuangalie miradi mingi sana tukizungumza mradi basi mradi ule hauwi kwa Unguja, mradi ule unakuwa Unguja na Pemba, na kuna miradi humu yote takriban ndio inayo-*cover* hapa Unguja na Pemba. Lakini ninachotaka kusema ukienda kwenye Kinga utaona ile *disbursement* ya pesa iliyotolewa utakuta iliyotolewa *almost* inalingana kwenye Kinga, lengo kuna tafauti pale, leo ilikuwa Unguja kubwa kuliko Pemba, lakini kilichotolewa chote 47,000,000,000/= ukiziangalia pale utaziona ziko wazi wazi kabisa, hakuna tafauti kwa sababu ya zile *activities* zenyewe.

Mhe. Spika, tuende kwenye uendeshaji lazima tukubali uendeshaji uko Makao Makuu zaidi kuliko Pemba, Makao Makuu ya Wizara. Kwa hiyo mapesa mengi yamewekwa pale kwa sababu ndio Makao Makuu ya Wizara, lakini Tiba nacho kimezidi zaidi ya Pemba, kwa sababu Tiba ndio kila kitu mpaka wagonjwa wa nje wote wapo kwenye Tiba, kwa hiyo ile kusema kwamba Pemba wananyimwa Unguja ndio wanapewa fursa si kweli, suala la Tiba ni sera ya Serikali, mambo yote yanayofanywa Unguja yanafanywa na Pemba, lakini *of course* tunakwenda kwa uwiano wa sasa takriban ya watu na uzito wenyewe wa masuala yanavyotokea.

Mhe. Spika, ukizungumza masuala ya kichocho, masuala ya kichocho kwa vyovyote Pemba yana kipaumbele kuliko Unguja. Sasa ningeliomba sana Waheshimiwa wenzangu watufahamu kwamba hakuna lengo hilo la ubaguzi wa aina hiyo, tunakwenda kwa mujibu wa matokeo yake, tunakwenda kwa mujibu wa vipaumbele vya Wizara na vipi pesa inavyopatikana.

Lakini la mwisho kabisa Mhe. Spika, suala la maslahi. Mhe. Rais au Serikali kwa ujumla siku zote imekuwa inapenda iwape kwa sababu *mcheza kwao*

hutunzwa, iwatunze vizuri madaktari wetu, tuwape na wao wajisikie wako nyumbani, sasa keki tu haituruhusu matatizo kidogo ya fedha sio kidogo makubwa hasa, tungependa sisi kimishahara tu-*compete* na wenzetu walioko Bara lakini kidogo tunazidiwa, *resource* zetu ni chache. Sasa mimi nawapongeza sana madaktari wetu kwa kweli wanafanya kazi kwa kujitolea kwamba wao wanajiona wako nyumbani, wanasaidia ndugu zao, wanasaidia jamaa zao. *Of course* kweli mcheza kwao hutunzwa na sisi kama Serikali tunafanya kila liwezekanalo ili tuweze kwamba tunaweza na wao tukawaona kwa jicho la huruma. Mimi ningeliwaomba sana Waheshimiwa tuwape moyo madaktari wetu, tuwasaidie, tufuate taratibu zilizowekwa na Serikali, wao wenyewe wameweka wapi rufaa, wapi hospitali nyengine, tukijenga vituo tuwafuate kidogo tuone utaratibu wao.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kusimama hapa kujibu hoja za Wajumbe Wawakilishi kwa niaba ya Wizara ya Afya. Kwa kuanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa afya, uzima na nguvu za kuweza kusimama hapa kutetea Wizara hii ya Afya, kama tulivyopewa jukumu na Mhe. Rais, kwa kuniamini. Kwa hiyo ninafanya kazi yangu kwa nia njema, kwa haki, kwa usawa kwa kila kile ambacho nimekabidhiwa kukifanya.

Mhe. Spika, Pia napenda niwashukuru Wawakilishi wote waliosimama na waliokuwa hawakusimama, waliotoa michango yao kwa maneno na walioandika, michango ni mingi na ushauri mwingi mzuri, najua hatutapata nafasi ya kutoa shukurani kwa mtu mmoja mmoja lakini karibu wote nilichoshukuru kwamba wametuona kwamba kazi tunayoifanya ni kubwa, ngumu na tunachokipata hakitoshelezi.

Kwa hiyo kama tungekuwa tunakipata kinatosheleza tupate kikubwa zaidi. Mimi napenda niwahakikishie kwamba kwa hicho tunachokipata tutajitahidi na Serikali inajitahidi kutupa kadiri ya kile inachokuwa nacho, na sisi tunakitumia kwa uadilifu kuhakikisha kwamba mambo yote yanakwenda vizuri.

Mhe. Spika, nawashukuru wazazi wote na jamii yote kwa kuitikia wito huu kwa kuja hospitali na kutuonesha kwamba wanahitaji zile huduma kwa kuwashughulikia kwa umakini, na ni hicho tu ndicho kitakachowafanya wao waweze kupona, wasipoteze maisha.Tumeukubali wito huu, tumeziona changamoto, tumetathmini baada ya mwaka mmoja tumejua tatizo liko wapi, kadiri tunavyokwenda tutajipanga.

Mwaka huu tunategemea mambo yatakuwa mazuri zaidi na yatakapokuwa mazuri zaidi tutapata changamoto, changamoto haziji, mwaka ujao tutazirekebisha, lakini itafikia wakati itatulazimu, kwa sababu kuna taratibu tafauti, uagizaji wa dawa una tafuati, na mengine mengi ambayo tumejipanga kuhakikisha kwamba agizo la Rais, kama kuna mtu ambaye hawezi kukataa agizo la Rais kulitimiza, tutalitimiza kwa asilimia 100 kama matumaini yake yalivyo, kwa sababu alinikabidhi mimi kwa ajili ya kufanya kazi.

Mhe. Spika, huduma za *emergence* zipo ingawa ni kidogo, lakini mradi wa ORIO tutajenga *section* kubwa kwa ajili hiyo.*ORIO* tunategemea itaanza shughuli zake, sasa hivi wakandarasi wanatafutwa na mengineyo ya utaratibu yanafanya, ndio hayo aliyosema Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi serikali imelipa asilimia 50 na wao watalipa asilimia 50, maana ndio miradi ya afya sasa hivi. Kwa hivyo, kama ni shilingi milioni 50, 25 serikali yetu 25 wao. Kwa hivyo, kitajengwa kitengo kikubwa, kizuri na kitafanya kazi masaa 24 kwa ajili ya *emergency*.

Kulikuwa na lawama ya wanafunzi kuchukua mazoezi Pemba. Mhe. Spika, Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja ndio peke yake inayotoa mafunzo kwa wanafunzi wengi, wasimamiaji ni wachache, madaktari wanaotakiwa wafanye ile shughuli katika hospitali ile saa 24 wako kwenye shughuli, muda ule umekuwa hautoshi tatizo hilo tumeliona. Na sisi kama Wizara na Chuo cha Afya Mbweni tunajipanga, na tumeshatayarisha mpango wa kuhakikisha kwamba tunapata wasimamizi wa kutosha tuwatafute baadhi ya wafanyakazi tuwalipe kwa ajili ya kazi hiyo na walimu wao, ili wale wanafunzi waweze kusimamiwa.

Mhe. Spika, ningependa kuzungumzia suala la vyakula Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kalizungumza nashukuru kwa hivyo sitolirudia tena.

Lakini uboreshaji wa maslahi ya wafanyakazi. Mhe. Spika, mimi ni mmoja katika waliokuwa wakigombana sana nilipokuwa sijawekwa katika nafasi hii. Kwa nini tunanyimwa? Kwa nini hatupewi *uniform*? Kwa nini hatupewi pesa za likizo na si peke yangu na wote hao unaowaona huko nyuma wote ni madaktari.

Kuna mtu hapa alisema kwa nini madaktari wanachukuliwa wanapelekwa juu huko wasikae tu hospitali wakafanya kazi, ili Wizara ya Afya iende lazima madaktari waweko juu maana wao ndio wanaojua shida zao, ukituwekea mtu yeyote akija mtu ambaye anazungumzia mambo ya afya kwa lugha ya Afya mtu wa kawaida hatofahamu, ina maana tena aweko na mkalimani pembeni, haina raha. Kwa hivyo, tuachieni tujimwage madaktari ndio nafasi zetu, kule

ndiko tunakotakiwa kuweko kutetea maslahi ya madaktari wenzetu na wafanyakazi wote wale.

Kwa sababu mfanyakazi yoyote wa afya kiongozi wake mkuu ni daktari, kwa hivyo msione tabu kwa wale walioko kule, tuna timu nzuri mno, tuna ushirikiano wa kutosha mno, sijui huko nyuma lakini mimi nashukuru kwa hilo. Tuko kule tumeshikamana na si kama wanavyosema watu kwamba hatupewi ushirikiano, Waziri hapewi ushirikiano kuna mengi ya mifano Mhe. Waziri baada ya kuweko pale kwa miaka miwili, miradi ni mingi iliyotekelezwa na ni mambo mengi yamefanywa.

Mhe. Spika, watu wote wanasema kwamba wengine wanatuonea wivu hapa mimi na Mhe. Waziri wangu jinsi tulivyo karibu. Kwa hivyo, hatuna matatizo sisi, siasa pembeni pale tuko kwenye kazi, tukitoka hapo kila mmoja huyu CCM, huyu *CUF* anakwenda kwake kusema anachokitaka, lakini kwa wizara ya kwetu ya afya hilo sisi hatuna, tunashukuru kwa hilo. Mhe. Juma Duni Haji nakupenda usishangae! *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika kutetea maslahi tumeweza sasa hivi angalau, tulikuta pale pesa za likizo hapana sasa hivi pesa za likizo zinatoka, kidogo kidogo sio nyingi lakini tunahakikisha kwamba kila anayekwenda likizo apate.

Uniform kila kitengo tutahakikisha kwamba wafanyakazi wanapata *uniform*. Linapokuja suala la *call* sasa hilo ndio hapo linapozua mzozo na suala la baada ya kazi, tunapofanya kazi za ziada (*overtime*). Kwa sababu lile liko katika *other charges* na likiweko kwenye *other charges* kinacholetwa tunakaa sote idara zote tunaangalia jamani tulichokipata hiki, tuangalie hapa bali *issue* ni nini, kile kinachohitajika haraka kama ni hiki kwa hiyo hicho tunaanza kukitengea, baadae kidogo kidogo tunagawana mpaka pesa zinafikia mwisho, sasa ukija ukiyatizama hayo yote unakuja kukuta kwamba daktari hapa *on call* haipo. Lakini unajua hilo ni muhimu kufanya kazi, lakini tulichonacho hakijatutosha hata yale yaliyokuwa ya msingi yako pale na yametushinda. Kwa hivyo, tunakuwa tunaweka pale lakini tunahakikisha, tunafuatilia Mhe. Waziri anaandika barua kwa Rais, kwa Mhe. Waziri wa Fedha, Katiku Mkuu wa Wizara ya Afya kila siku anapanda akishuka kuhakikisha kwamba pesa hizo tunazipata.

Lakini tukienda kule wakisema hakuna inabidi tukubali kwamba hakuna, lakini tunawaahidi kwamba hizo tutazifuatilia na kila mwenye haki yake atapata. Tuna ratiba yote ya madeni na hivyo wafanyakazi wetu tunaomba watuamini na tuko hapa kwa ajili yao na tutashughulikia.

Sisi tunapenda wapate, mimi nisingependa wala daktari mwengine kuona daktari mwenzetu hapati, haiwezekani ndio sisi sisi tuliokuwa tukilia tulipokuwa kule. Mimi nakuwa najiona *guilty,* na-*feel guilty* kwamba nashindwa kuwahudumia wafanyakazi wangu na wakati mimi niko pale, lakini kama sina cha kuwapa niwape nini? Tutajitahidi.

Kumezungumzwa hapa kuhusu afya ya Bandarini na uchunguzi wake. Mhe. Spika, bandarini na *airport* ni sehemu ambazo wageni wanaingia. Kwa taratibu za kimataifa wageni wote wanatakiwa tuhakikishe hawaingii na maradhi.

Tuna wafanyakazi ambao wakemia wako katika sehemu hizo, utakuta tu pengine labda *airport* kulikuwa hakukuwa na vyumba maalum vilivyojengwa kwa ajili hiyo na kule hakutakiwi vitanda, kule hakutakiwi dawa, anatakiwa mtu ambaye tunamtilia wasi wasi tuweze kumuweka pembeni, tumchunguze. *Set up* zipo, *thermometer* zipo, kama tuna wasi wasi tuite *ambulance* tumchukue tumpeleke kunakostahiki akachunguzwe ili kuhakikisha watu wetu wanakuwa salama.

Jana Bandari imefunguliwa tumepewa chumba kikubwa cha kutosha, kwa hivyo pale tutajitahidi kuweka huduma zote zinazostahiki ili maradhi yasiingie, na walioko pale wana elimu ya kutosha kuhakikisha kwamba meli zinazoingia na kutoka ziko salama.

Kitanda cha operesheni kimetajwa kwa wazazi kilikuwa kibovu kinapandiwa usiku na mchana lazima kibomoke, lakini tumeshusha chengine kutoka juu na tumeki-*replace* kile. Kwa hivyo, kilichopo sasa hivi ni kizima.

Hapa nataka nizungumze suala moja ambalo limesemwa kwa nguvu na watu tujaribu kuwafahamisha lakini bado hawataki kufahamu, au sijui wanatufanyia tu inda makusudi Waheshimiwa Wawakilishi wasitufanyie, sisi tupo kwa nia njema.

Suala la *insulin.* Mhe. Spika, mimi nafikiri ifike wakati ya Ngoswe tumuachie Ngoswe, sisi ni wataalamu naomba watuamini, wataalamu wa afya ni kama jeshi kuna Kamanda Mkuu, kuna Brigedia, kuna wengine unakwenda mpaka chini unakuta wale asakari wa miguu ndivyo tulivyo na kila mtu ana idara yake. Suala la dawa liko kwa Mfamasia Mkuu, sisi madaktari ni watumizi wa mwisho.

Mfamasia Mkuu ndiye anayechukua jukumu. Kitengo cha *tender* kinapofanya manunuzi kinamuita Mfamasia Mkuu kutaka ushauri hakiniiti mimi daktari kwenda kutaka ushauri. Mimi namwambia nataka dawa fulani aina ya chupa

nzuri na si nzuri, ya Uingereza na India hiyo si *issue*, kilichomo ndani ya ile chupa ndio muhimu na sisi kilichomo ndani ya ile chupa tunakiamini. Kwa hivyo, kama tunakiamini kwa sababu tuna *document* tele pale Waziri anazo zinakotumika hizo dawa.

Mhe. Naibu Spika, mfano mdogo tu *panadol* nenda dukani wewe au *pharmacy*, ukisema unataka *panadol* utaulizwa unataka ya Dar es Salaam, Unataka ya Kenya, India, Belgium au ya Uingereza? *List* kubwa. Kwa hivyo, dawa zinakotengenezwa ulimwenguni zote haziwezi zikatoka kama hazikuchunguzwa ipasavyo kwa *stage*, zinakwenda *stages* nne ndipo zinatiwa dukani. Tutahadhari sana tunapozungumza suala la dawa kwamba hii haifai, mwenye dawa yake anaweza akatushtaki ili tukatoe ushahidi kule jamani, chonde chonde tunapozungumza dawa!

Sasa hili la *insulin* kama kuna wagonjwa ambao wamepata *reaction* mimi nashangaa badala ya kuja hospitali walikopewa dawa wanakwenda kwa Mhe. Makame Mshimba kwenda kufanya nini. Dawa yoyote ile hakuna dawa iliyokuwa haina tatizo hata *panadol* kuna watu zinawadhuru, hata *chloroquine* kuna watu zinawadhuru, *SP* kuna watu zinawadhuru na nyengine. Kwa hivyo, na *insulin* kutatokea watu itakayowadhuru, waje hospitali tuna utaratibu tunaangalia watu wote wanaopata matatizo ya dawa, akifika pale anabadilishiwa dawa na ile tunaiweka kama kumbukumbu kuona tatizo ukubwa wake ni kiasi gani.

Hapa tumeshawahi kubadilisha dawa za Kifua Kikuu kwa sababu wengi walipata matatizo na tukiona dawa inawapa matatizo watu wengi tunaibadilisha, na tukiona dawa inampa mtu matatizo anakuja kule anapewa *anti dose* ili lile tatizo liondoke. Kwa hivyo, tusiende huku kwa wasiokuwa madaktari wanaotaka udaktari.

Kumezungumzwa hapa suala la *pharmacy*, Pemba hakuna *pharmacy*. Mgao utakaokuja una ma-*pharmacist* na si kwa ma-*pharmacist* tu, mgao ujao wa wafanyakazi kwa kiasi kikubwa utapunguza upungufu wa wafanyakazi. Mimi nasimamia ugawaji wa wafanyakazi sichagui Pemba sichagui Unguja, naangalia vituo vyangu vya kazi vipi havina wafanyakazi nipange, siangalie katoka Unguja wala Pemba. Sasa wale wanaokaa kule wakafikiri kwamba mimi nitakwenda kumwambia Dr. Sira mwanangu asimpeleke Pemba asije hivyo, mimi napanga mtu pale ambapo hapana wafanyakazi. Tunajua kwa sababu tuna *minimum requirement* ya wafanyakazi wetu, tunajua upungufu wetu ulipo na tunapanga kwa mujibu wa mahitaji na kipi kitakachobakia kinatakiwa kijalizwe tunakifahamu.

Mhe. Spika, mtu anayejua taarifa zake zote anaweza kupanga vizuri, kama mtu hana taarifa ya shida zake akajua wapi pana mahitaji kiasi fulani hatoweza kujipanga. Lakini Wizara ya Afya tuko mbele kwa hilo na tunajidai tuko kifua mbele tunajua mahitaji yetu.

Hapa kuna suala la watu ambao wamepata matatizo kwa mfano *TB* lakini hawaangaliwi. Mimi nasema hilo si la kweli, mimi nimefanya kazi Kitengo cha *TB* pale kila mwaka watu wanafanyiwa *check up* kwa sababu tunajua kwamba ile ni sehemu nyeti, mtu anayekuja na *TB* wanampumulia daktari. Kwa hivyo, yeye pale ndio anapata *dose* kubwa. Sasa pale kila mwaka tunaweza baada ya miaka miwili tukapata mtu ambaye tayari amepata tatizo, hapo hapo tunamtibu na anakwenda Kitengo cha *occupational therapy* kule kufanyiwa taratibu za malipo yake. Watu kama hao ndio wanaotakiwa wapewe *risk allowance*, ni kweli tunakubali *risk allowance* lakini *risk allowance* sio ya kila mfanyakazi wa Wizara ya Afya. Dereva *risk allowance, orderly risk allowance*, kuna *specific area* ambazo zinatakiwa zipewe *risk allowance* na tunazipigania na *Inshaallah* pengine safari hii tutakuwa nazo na tutawapa wanaostahiki.

Kesi za UKIMWI watoto wako wengi tutawafanyaje, tunawatizama vipi hatma yao. Sisi kama hospitali kazi yetu ni kuhakikisha wanapata dawa hayo mengine ni ya Ustawi wa Jamii. Kama tumelisikia hilo tutalichukua tuone tushauriane nao vipi wenzetu waweze kuwasaidia watoto hawa, lakini kuna Kitengo cha *ZAPHA*$^{+}$ pia kina huduma nzuri kwa wote wale wenye UKIMWI, kwa hivyo hao nao pia wanachukua watoto hao.

Kuna maradhi ya Ukoma hapa yalitajwa wagonjwa wanatembea tembea ovyo. Nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba bado angali ana mawazo ya kizamani, ulimwengu umesonga mbele zaidi. Mgonjwa wa ukoma leo hatishi kama mgonjwa mwengine, hatuna haki ya kumnyanyapaa, hatuna haki ya kumsusa, hatuna haki ya kufanya hayo tunayotaka kuyafanya; akishalemaa akikatika vidole havirudi atabakia mlemavu, sio mkoma hapana, ni mlemavu wa ugonjwa wa ukoma. Sasa mgonjwa wa ukoma tukimgundua leo hii ukianza kumpa dawa baada ya mwezi mmoja mgonjwa yule haambukizi tena, kwa hivyo hatuna sababu ya kuwafungia ndani kama wako jela, tuwaache watembee kama wanavyotembea watu wengine na haki zao kama binadamu wapate.

Kingine ambacho ningependa kukisema kimetolewa hapa kama ushauri, wanasema elimu ya afya kwa njia ya TV na Redio haifiki kutokana na matatizo tofauti yaliopo. Nataka nikubaliane na hili na tumeshauriana kwamba elimu ya afya ya uso kwa uso kupitia njia nyengine ngoma, magari zifanyike yale ndio yanayowavuta watu wakasogea. TV siku hizi kuna vipindi

vingi mno mtu akisikia afya tu kazima puu, anafungua kwengine, redio akifungua akisikia afya anazima anaitafuta *Bongo flavour*. Kwa hivyo, elimu haifiki kweli nakubaliana na yeye kwa hiyo tutatafuta njia zilizo bora.

Lakini pia hapa pamezungumzwa suala la maradhi yasiyopewa kipaumbele, wengi wamelizungumzia. Ninachopenda kusema jamani hilo ni jina tu, limetolewa na *WHO* kwamba maradhi hayo huko nyuma yalikuwa hayakupewa nafasi, tulikuwa zaidi tunatoa nafasi kwa maradhi ya kuambukiza. Kwa hivyo, ndio maana ukakuta TB, UKIMWI, Malaria yale ambayo yanaambukiza ambayo yalikuwa ni tatizo kubwa katika nchi zetu na mataifa yaliyo makini.

Sasa matatizo hayo kwa kiasi kikubwa yamepata ufumbuzi kwa hiyo sasa ndio tunageukia kwa yale maradhi ambayo tunasema hayakupewa kipaumbele, ndio tukija huku kama kichocho, minyoo, matende, haina maana hayatibiwi; kazi inafanyika lakini sasa kuna maradhi 17 ambayo huko nyuma yalikuwa hayakupewa kipaumbele sasa *WHO* wameyageukia hayo na hayo sasa ndio tunayafanyia kazi. Kwa hivyo, tunachokusudia hapa ni jina tu lisiwashtue isipokuwa kazi inafanyika, kichocho kitatibiwa na tuna mipango madhubuti, kuna tafiti zinafanyika na tuna mpango wa kuhakikisha kwamba kichocho, matende, minyoo Unguja yawe ni historia kama vile ambavyo malaria yamekuwa.

Wachina wamekuja kwa nguvu zote, unajua wakubwa wakikinaiana mambo yanakuwa mazuri, Wamarekani na Wachina wanashindana hapa faida iko kwetu, kila mmoja atachukua fungu lake.

Mhe. Spika, nafikiri nizungumzie kidogo hapa kuhusu suala la Mhe. Asaa Othman Hamad, chochote kinakwenda *in charge*, katuvunja moyo mno. Jamani! Kweli Unguja na Pemba tukatengane kwa maslahi watu wasome kada moja, walipwe maslahi tofauti, tulinganishwe kwa mishahara, tulinganishwe kwa pesa zinazopata Unguja na Pemba, si kweli! Unguja ni Makao Makuu lazima tutambue hilo, kuna Wizara na Idara zote Unguja. Fungu lile la Unguja linachukua wizara halafu inakuja Unguja yenyewe na Pemba inakuwa ilivyo, ukishatoa fungu kubwa la wizara siku zote sisi tunasema mmh, Unguja tunapata kifungu kidogo kuliko Pemba na kama uongo wako pale juu na waseme, wanayoyafanya Pemba Unguja hatuwezi kuyafanya kwa sababu pesa zetu zinakuwa kidogo, na hizo za Unguja za Makao Makuu haziwi za Unguja zile ni kwa Unguja na Pemba Mhe. Spika, iwe miradi au iwe kitu chengine.

Kwa hivyo, jamani msiwape watu fikra kuona kwamba tunanyanyasana katika visiwa vyetu hivi. Ni mbaya, ni mbaya, sumu ile ya ubaguzi

tunayoieneza kwenye Baraza hili la Wawakilishi ni mbaya. Chagueni ya kusema hivyo, vyenginevyo tutaiweka nchi yetu kwenye matata. Sitaki kusema kimoja kimoja alichokisema kwa sababu vyote vilikuwa vinazungumzia hayo kwamba tunabaguana, hatufanyi hivyo!

Mhe. Spika, nafikiri hapa nizungumzie suala jengine linalozungumzia Katibu Mkuu wetu. Katibu Mkuu wetu wenyewe tunamuamini ni mahiri, ni mtafutaji, ni mhangaikaji. Tumeambiwa hapa anasafiri, jamani pitieni wizara zote mkaangalie Makatibu Wakuu hawasafiri kule wanasafiri wa afya tu? Si kweli Makatibu Wakuu hilo ni moja katika majukumu yao kuhangaika kutafuta. Nimeangalia safari za mwaka jana ambapo mwaka huu wa fedha tunaokwenda nao, sisi katika bajeti yetu tunachokipitisha kifungu ni kimoja tu kwa ajili ya safari za Katibu Mkuu na Waziri wake kwenda Geneva kwenye *World Health Assembly*, kwenda kwenye mkutano huu kulikobakia kote wafadhili, ni maombi, ni mialiko.

Katibu Mkuu kasafiri mara tisa. Katika mara tisa hizo pesa za serikali zilizotumika ni hizo tu za *World Health Assembly*, kwengine kote aidha ataitwa akatutetee, aidha ataitwa akatoe maelezo, aidha ataitwa akatoe ushauri na inabidi aende ili hayo tunayoyahitaji akatutafutie. Tusimuweke pabaya Katibu wetu hayuko hivyo.

Kuna jambo lililozungumzwa hapa la wakunga wa kiume katika wodi. Tatizo la wafanyakazi wa afya ni la dini, na kila kukitokea tatizo inabidi kubuniwe mitindo itakayoweza kuiwezesha afya iweze kufanya kazi. Zamani tulikuwa tunagawa manesi watasomeshwa kuzalisha, wanaume watasomeshwa maradhi yao mengine na maradhi ya magonjwa ya akili.

Katika upungufu wa wafanyakazi mitaala ya ulimwengu imebadilika; wanaume na wanawake wote wanasomeshwa kitu kimoja ili popote watakapokwenda waweze kutoa huduma zote kwa wanawake na wanaume. Iweje madaktari wote wanaoshughulikia wanawake ni wanaume leo mwanamme akizalisha iwe tatizo? Tukitaka tusitake lazima tukubaliane na mabadiliko ya ulimwengu si amri yetu sisi, ni upungufu wa wafanyakazi.

Chuo cha Afya Mbweni sasa hivi hakisomeshi manesi wanaume na wanawake tofauti kuna mtaala huu mmoja ambao unayachanganya yote. Kwa hivyo, naomba tukubali mabadiliko tusiwe *rigid* kama vile tumeandikiwa kwenye msahafu. Lazima twende na mabadiliko tukiambiwa tubadilike, tubadilike, na tunabadilika na ulimwengu.

Hapa kuna suala lililozungumzwa kuhusu matatizo ya macho. Kuna madaktari hapa wanatakiwa tunakubali, tumesomesha wameondoka

tunajipanga tutawasomesha kwa sababu mahitaji tunayajua yapo. Na hii nataka nikwambieni kuna kitu kimoja, hapa watu labda wana-*refer* kuna wakati fulani kulifanywa Hanyegwamchana kule uchunguzi wa macho wakakutikana watu wengi wana matatizo ya macho. Watu wazima wowote ukishafikia umri wa miaka 40 wengi wao asilimia kubwa uoni wao unapungua. Kwa hivyo, kukutwa na tatizo kama hilo katika umri huo ni jambo la kawaida. Na sisi tunaotumia makaratasi na kompyuta ndio kabisa macho yetu yanapungua nuru haraka sana kwa sababu ile ni mionzi. Kwa hivyo, hilo sio tatizo tunalifahamu na huduma watapewa wa miwani atapewa.

Mhe. Spika, kuhusu Maabara ya *PHL* haipewi pesa. Nimekuwa kwenye mkutano kama mliona hapa kuna kipindi kifupi sikuwepo kwenye Baraza, tulikuwa Geneva kwa ajili ya hilo, kile kitengo kina-*generate* pesa kiasi ambacho kinaisaidia wizara, kinasimamia *PHL*, kinalipa Micheweni, kina kila kitu kina uwezo wala hawazihitaji pesa zetu maana wanajua hatuna. Na katika Kamisheni iliyopitishwa hicho kipengele kimeshaondoshwa kabisa, sasa *PHL* tumeipa jukumu kwamba isimamie afya ya jamii ya Zanzibar. Kwa hivyo maabara zote isimamie, tafiti zote isimamie na pesa pia watupe maana wakiwa nazo nyingi watupe sisi ili tufanye mengine. Kwa hivyo, suala la kwamba tuipe *PHL* katika mkataba wa mwanzo lilikuwepo ilipoanza, lakini matokeo yake imeweza kufanya vizuri na inapata fedha za kutosha kuweza kujiendesha na kuiendesha wizara.

Matatizo ya Kensa ya Kizazi yamezidi. Mhe. Spika, tunapata matatizo ya kensa wagonjwa wapo, lakini ili tuweze kusema hivyo tunahitaji tafiti zitakazotupa *data* za kusema hili ni tatizo. Matatizo yapo hatukatai lakini kwa wingi kiasi gani lazima tufanye utafiti. Kitengo cha Kensa kinaandaliwa tuko katika mchakato na mwisho wake tutapata usajili ambao utakusanya watu wote wenye matatizo tutatoa kwa uwazi kwamba tuna tatizo kubwa kiasi gani, na tutajipanga tuanze kufanya huduma kwa kiasi gani. Kwa hiyo, tusubiri kidogo tuko katika taratibu za kulishughulikia hilo, lakini kwa sasa siwezi nikasema mengi kiasi gani au yamezidi kiasi gani, kwa kweli tutakuwa ni waongo, sisi hatusemi vitu bila ya *evidence based* ya *data***.** Tupate *data*, tufanye utafiti tuseme.

Watu wakijifungua wanapewa lugha siyo. Najua Wizara ya Afya tuna *challenge* nyingi juu ya lugha za wafanyakazi wetu ambazo zinalalamikiwa. Lakini sasa, tatizo liliopo kama zile kesi za watu kubakwa ukimwambia mtu toa ushahidi, njoo useme, anayekutolea maneno kamsemee tuchukue hatua hawataki sasa tutalitatua vipi tatizo hilo? Hebu kila yule anayepata tatizo aseme waone kama hatutochukua wafanyakazi, lakini tukizunguka tukisema pembeni na kwenye redio na magazeti hiyo haitusaidii kwa sababu sisi hatuna ushahidi mkononi, wanaposema huko sisi hatupo, ukija ukitushtakia

tukikwambia mtaje mtu jina unakimbia unaanza kujizungusha. Mwenye tatizo atakayetolewa lugha mbaya aseme,na ana haki hata ya kushtaki kwa sababu kadhalilishwa!

Kwa hivyo, nasema wafanyakazi wangu jamani nasema kwa kinywa kipana, maadili yetu hayaruhusu hivyo, na mtu akija akishtakiwa asiseme Naibu Waziri kanifanyisha nikashtakiwe, ni lugha yako na mdomo wako. Mimi nimefanya kazi zaidi ya miaka 35 nataka mtu yeyote aseme hapa leo au huko katika Visiwa vya Unguja na Pemba kwamba Dr. Sira aliwahi kunitolea neno lapata hivi! Nayajua maadili yangu sijawahi kumtolea mtu maneno, na kama yuko ajitokeze kwenye kisiwa hiki sijawahi. Naomba muwe mfano na ndio maana nimewekwa kama kiongozi wenu tufuateni tufanyeni mazungumzo.

Kuna Suala la Daktari wa Kikorea na Kituo cha Rahaleo, lakini cha Rahaleo kitazungumzwa katika vituo vyote. Lakini suala la daktari wa Kikorea Mhe. Spika, tumelichukulia hatua, tumelichukulia hatua kuna *document* hizi hapa, wamekwenda, wametizama, tumeshawaita watu wa tiba ya asili, wao wenyewe kitengo chao na *NGO* yao imeshaandika barua na hatua zinazidi kuchukuliwa, wameonywa kwa maandishi. Sababu ya kifo haikuwa yao, lakini kwa kuwa walipita kwao ndiko kunako tatizo, kama unazihitaji Mheshimiwa hizi hapa *document* zote kuhusu hiyo kesi.

Chengine ambacho ningependa nikiseme hapa kuhusu Mnazi Mmoja na watu kutolewa. Napenda nikubali sisi wizara tulikuwa tunajipanga tufanye utaratibu wa kuwatoa watu Mnazi Mmoja wakati tumeshajiandaa katika kuwapeleka wapi, lakini kwa bahati mbaya tu na kwa matatizo makubwa yaliyokuweko Mnazi Mmoja na watu walivyokuwa wanasongamana, na watu walikuwa hawataki hata kwenda vituo vyengine lazima waje kule hata kama dawa ziko kule wakazidiwa mno, wakaona hapa cha kufanya tuwatoe, wakafungua Kituo cha Rahaleo lakini bahati mbaya kituo ni kimoja, bahati mbaya kituo kinafanya kazi mpaka saa tatu usiku.

Tunachosema kwamba kuanzia saa tatu watu wanaweza kwenda Mnazi Mmoja, Jumamosi na Jumapili watu wanaweza kwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa sababu vituo vingine havifunguliwi. Lakini tukijipanga tutakuwa na vituo vingi ambavyo viko katika matayarisho *DANIDA* inavitengeneza na wafanyakazi tumeshawaandaa wa kwenda kwenye vituo vile.

Mhe. Spika, Mpendae itafanya kazi masaa 24, Sebleni, Kwamtipura, Rahaleo, Kituo cha Jang'ombe na Kituo cha Chumbuni. Tumeangalia jiografia ya mji wetu ili kila mtu apate pa kufika hakuna anayetaka kuja Hospitali ya Mnazi Mmoja usiku lakini hakuna kituo cha karibu, lakini hivyo vikifanya kazi saa

24 tutakuwa hatuna tatizo na Mnazi Mmoja watakaokuja watakuja na karatasi maalum ya rufaa kutoka kwenye hivyo vituo kuja kule kwa ajili ya matibabu.

Kwa hivyo, naomba radhi sana wale waliopata usumbufu, nia haikuwa hiyo mtusamehe kwa hilo, lakini mjue kwamba nia yetu, nasi kwenu hatutaki mpate shida na tunajipanga vizuri ili kuhakikisha kwamba huduma zinakuja karibu yenu.

Mental imezungumzwa tumeambiwa hakuna hata daktari. Daktari keshakuja yupo na kitengo cha Pemba kitafunguliwa mwezi ujao tukijaaliwa na madaktari walioko Pemba wapo na wagonjwa wapo. Tizameni kwenye kitabu nyuma kule *list* ya wagonjwa wa Pemba ipo waliotibiwa na wanaendelea kutibiwa.

Kwa hivyo, nafikiri hilo sio tatizo kubwa, wafanyakazi safari hii tumewapanga hospitali zote zitakuwa na wafanyakazi. Kabla hatujawapangia vituo tumehakikisha kwamba vituo hospitali zitakuwa na wafanyakazi, sasa watakaa au hawakai hilo ni suala jengine.

Nilikuwa nataka niwapongeze wale waliosema tuongezewe mishahara. Tunastahiki lakini haliko kwenye mamlaka yetu, lakini Serikali inatoa walichonacho. Sasa kama tunakaa tukae kama sisi tulivyokaa, sisi tumesomeshwa na Serikali hii na tumekaa, kwa hiyo tukalie moyo na uzalendo na hayo mengine yafuate baadae.

Lakini aliyekuwa hana moyo, hana uzalendo, akiondoka sawa kama anataka mamilionea atakwenda Bara, wale wana dhahabu wana kila kitu, hivi keshokutwa wanachimba gesi sisi tuna nini baada ya matofali ya chokaa, ndio tunachokichimba. Kwa hiyo, jamani tukaeni wafanyakazi tuwahudumie ndugu zetu kweli kila mtu anapenda maisha mazuri.

Hapo Chuo cha Afya hao wanaosomeshwa kila siku si wanalipa, wanalipa asilimia 60 Serikali inaongeza asilimia 40 basi hata hilo hamfikiri, tukaeni tuwahudumie ndugu zetu. Si hivyo kila anayetaka kuondoka kabla hajaondoka ili tumpe cheti chake tutawambia kwanza tulipe asilimia 40 iliyobakia ukishatulipa chukua cheti chako nenda zako. Tuangalie na hawa na wao wamezaliwa kuwaacha ndugu zako wanakutegemea wewe na wamekupeleka Chuoni halafu ukawaacha ukatokomea unakotokemea.

Nilikuwa nataka nizungumze suala alilozungumza Mhe. Mwajuma Faki Mdachi habari ya hawa kutopewa haki zao. Nilikuwa nataka kukwambia hivi kwamba tunapopima ukimwi tunapata majibu mawili ndio au sio. Kwa kipimo hicho tunaweza kumsikiliza sasa hili si jambo jepesi kumwambia

kuwa mtu ana ukimwi lazima atape mtu akae kitako amwabie yule mtu akakubali, afahamu kwamba huu ndio ulimwengu haya yametokea huuguwi peke yako anaugua kila mtu, dawa zipo usiwe na wasi wasi mpaka ile roho yake iridhike.

Ndipo sasa unamwambia kwa bahati mbaya sana umeathirika na ndio maana tukimuona mtu mwepesi tunamwambia kamuite mzee wako au ndugu yako ili tupate *support* ya wazee kwenye lile. Kwa hiyo ni taratibu sio kama tunawacheleweshea.

Nafikiri baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nirudie tena nawashukuru wale wote Mawaziri waliotilia mkazo na namwachia Mhe. Waziri wa Afya Mhe. Juma Duni Haji achukue nafasi yake. Naiunga mkono bajeti hii asilimia mia moja. (Makofi).

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naanza tena kwa *bismillahi rahmaani rahiim*.

Nashukuru tena kupata nafasi kuja kutoa baadhi ya maelezo ya michango ya Wajumbe, na ningeanza kwa kushukuru sana kwa michango iliyotolewa na Wajumbe wasiopungua 25. Na kila mmoja ameeleza alivyoweza kueleza wengine wameeleza kwa ushauri, wengine wameeleza kwa kukosoa, wengine wameeleza kwa hamasa kubwa ndio wajibu wao. Kwa sababu yanayotokea mengine si mazuri kwetu yanawaathiri jamii yetu na hasa suala la afya.

Nawashukuru nyote na naomba kuhakikishieni kwamba hatuna kinyongo na mtu yoyote niwajibu wetu sote kushirikiana kutekeleza yanayotuhusu.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza ni vizuri kuwatambua wale waliochangia ukimwacha Mwenyekiti wa kamati, kuna wengine ni kama hawa:
Mhe. Jaku Hashim Ayoub
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Suleiman Hemed Khamis
Mhe. Asaa Othman Hamad
Mhe. Abdalla Juma Abdalla
Mhe. Ismail Jussa Ladhu
Mhe. Kazija Khamis Kona
Mhe. Abdalla Moh'd Ali
Mhe. Salma Mohammed Ali
Mhe. Nassor Salim Ali
Mhe. Mussa Ali Hassan
Mhe. Viwe Khamis Abdalla
Mhe. Salmin Awadh Salmin

Mhe. Salma Mussa Bilali: Huyu amefanya mambo mawili ameleta kwa maandishi lakini akapewa nafasi na Mhe. Spika, aelezee vile vile
Mhe. Mwajuma Faki Mdachi
Mhe. Panya Ali Abdalla
Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, Waziri wa Nchi OMKR.
Mhe. Mohammed Said Mohammed, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Huyu nae amechangia kwa maandishi.
Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini,Waziri wa Nchi, ORMBLM.
Mhe. Naibu Waziri wa Afya

Na mwengine walioichangia kwa maandishi ni hawa:
Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
Mhe. Shadya Mohamed Suleiman
Mhe. Marina Joel Thomas
Mhe. Farida Amour Mohammed

Wote kwa pamoja nawashukuru na kama kuna niliyemsahau naomba aniwie radhi, mimi ni binaadamu nimeshindwa kumuorodhesha.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya mambo mengi ambayo ameeleza Mhe. Naibu Waziri wangu namshukuru sana kwa sababu mengine ni ya kitaalamu ameyafanyia uchambuzi wa kitaalamu yeye ni daktari wa utaalamu mimi si daktari, mengine ni ya utawala amenisaidia.

Sasa kuna njia mbili, kuna mambo takriban watu wanasema Mtambuka; wengi wameyaeleza ingawa kila mtu alivyotaka kuyaeleza. Hoja kubwa zilizoelezwa ambazo zimekwenda kwa wachangiaji wengi ni suala la upungufu wa dawa, suala la uzazi na mama kutoleshwa fedha, suala la upungufu wa wafanyakazi, suala la mishahara ya madaktari, suala la motisha, na suala la kuwatizama wagonjwa na kubwa kuliko yote ni suala la bajeti.

Naomba hili la bajeti niliseme mwisho na haya mambo 7 au 8 ningeyaanza mwanzo na halafu nitapitia maoni ya Wajumbe yale ambayo naona nahitaji kurudia, nitakalolisahau mtapopiga buti mnaweza kunambia kuwa hapa Mheshimiwa ulisahau.

Suala la dawa ni kweli kwamba kumekuwa upungufu wa dawa, lakini upungufu wa dawa hata tulipoingia Serikalini tumeukuta upo na kwa miaka mitatu sasa nikisimama mbele yenu hapa katika changamoto ambazo huwa nazisema ni moja katika upungufu wa dawa. Kama mnakumbuka vizuri bajeti nilizokuwa nikisema fedha za dawa kwa jumla zilikuwa chache. Lakini kila mara nilipokwenda Serikalini ninapokuja kuzungumza hapa zikawa zinaongezwa. Zilianza na milioni kama mia tatu zikaenda mpaka milioni mia

saba mwaka jana, tukapewa bilioni moja na laki tano na mara hii tumetengewa 2.1 bilioni.

Sasa hiyo kwanza inaonesha kwamba wale tunaowaeleza wameanza kuliona kwamba suala hili ni muhimu. Kidogo kilicho tofauti ni kwamba kutengewa na kuzipata fedha, na kuzipata fedha ni kutokana na aina ya bajeti tuliyo nayo. Bajeti tuliyo nayo wenzangu mimi najua a, b, c najua *cash budget* tuchume kwanza halafu tutumie, kama vile tunavyopata mishahara yetu mara nyengine unaombwa unaambiwa kuwa uje mwisho wa mwezi.

Sasa *cash budget* inategemea ukusanyaji wa *revenue*. Kwa hiyo, mara nyengine tunakuwa hatupati kama tulivyotegemea. Mimi nina picha ya Bajeti nzima ya Serikali kwa sababu nimo kwenye *Cabinet* kwa wastani yoyote ilikuwa ni utekelezaji wa 60% ya *target* na mkitizama na wizara nyengine nyingi mtazikuta hivyo hivyo.

Lakini pia tusisahau kwamba kulikuwa na pesa zimetengwa kwa ajili ya meli na ilikuwa kusemwa na Waziri wa Fedha hapa ikabidi zile zikapelekwa huko. Kwa hivyo suala la dawa kwa kuanzia ilikuwa ni suala ambalo linapelekwa Serikalini tunalizungumza kwenye *Cabinet* tunalieleza na hata tunamuandikia *memo* Rais kwamba Mhe. Rais baada ya mishahara sawa na wengi walikuwa wanaotusaidia wafadhili hasa *DANIDA* ni dawa.

Sasa kitu kizuri kwamba kwa mwaka huu tumetengewa 2.1 bilioni. Lakini katika hizo harakati alizosema Mhe. Naibu Waziri wangu kwamba ni changamoto ya *process* ya kubadilisha haya matatizo, maana moja katika changamoto ya kubadilisha matatizo Mhe. Spika, sio suala la shkamoo maharaba hapana; ni suala linaloendelea, tumehakikishiwa na tumekubaliana mpaka kwenye *cabinet* na si vibaya kumnukuu Mhe. Rais anamwambia Mhe. Waziri wa Fedha 2.1 bilioni kwa dawa hazina hoja yaani si suala kwamba pesa huna Waziri wa Fedha mwenyewe akasema kwamba Mhe. Rais hii hakuna nenda uje.

Kwa hivyo, *at least* hiyo tumehakikishiwa kwamba suala la dawa kwamba litapungua kwa kiasi kikubwa hakuna nenda uje, na katika hivyo tumekubaliana basi katika kulikabili kwamba tutafungua *account* ya dawa maalum ambayo tutashirikiana na *DANIDA* na wao wako tayari kutia 1.5 bilioni kwenye *account* hiyo, na Wizara ya Fedha mwezi huu wa Julai wanatakiwa watie 500 milioni *account* inaanza kufunguliwa na bilioni 2 ya dawa, na dawa hizo tumezifanyia uchambuzi tukagundua kuwa kuna dawa 100 zinatumika tangu kituo cha *Primary health* mpaka Mmazi Mmoja yaani zile *general; panadol* na kadhalika. Wenyewe wanajua sitaki kutukana utaalamu niliokuwa siujui. Lakini kuna dawa 100 ambazo hazitakosekana

popote utakapokwenda hilo la kwanza. Dawa nyengine ambazo zinahitajika kwa mahospitali makubwa nazo pesa zake zitakuwa ni zile zilizobaki.

Pili ni kwamba unununzi tuliokuwa tukinunua dawa na nimeueleza kwenye bajeti kwenye sehemu ya *pharmacy* tukinunua dawa *MSD Medical Store* Dar es Salaam mnalijua dudu lile Mhe. Makame Mshimba kwenye kule wana matatizo taarifa tulizonazo, na mpaka kwenye Bajeti ya Muungano wanaidai Serikali ya Muungano hawajalipwa na Serikali. Matokeo yake kule sasa ni mkorogovyogo na kama mnakumbuka ikatokea ile *issue* Katibu Mkuu wa Afya akaondolewa kwa sababu ya madudu kule.

Mhe. Spika, nimeletewa karatasi nilimsahau Mhe. Subeit Khamis Faki samahani sana.

Kwa hivyo, hatutonunua tena dawa hizi 100 *MSD* tutatoa tenda *International Tender* na mtaalamu wa kufanya kazi hiyo katika taratibu za *World Bank* si taratibu za Makame na Pandu, taratibu za *World Bank* tutoe *International Tender* kwa mfumo wa *contract,* tukipata dawa hizo isiwe ni fulani kapata kumi au kapewa mbili itakuwa hakuna sisi tunasema *account* yetu hii hizo hapo bilioni 2 tenda inatayarishwa kwa msaada kutoka *DANIDA* wamekubali.

Kwa hivyo, nategemea Mhe. Spika, suala la dawa katika mwaka ujao halitokuwa kama lilivyokuwa mwaka huu. Na nimeeleza humu kwenye bajeti tatizo lililotupata kuhusu dawa ni kwamba dawa tunaagiza za kuja Januari zinafika Mei, na zilipofika Meli asilimia 40 ya zile tulizotaka, mkorogano, lawama, katika hali hiyo ndipo tunapokimbia sasa Wizara ya Fedha maana yake itakuwaje tunatoa tenda, baada ya kuzipata dawa inakuwa tayari watu leo hakuna dawa bwana Juma hupigiwa simu mpaka nikaizima mimi wengine wananambia kuwa nafanya jeuri sipokei kumbe nimeshachoka masikio yanauma.

Kwa hivyo, ndugu zangu suala la dawa watusamehe sana kwa ukosefu lakini tumo katika kubadilisha mfumo mpya, na mabadiliko haya yatachukua muda changamoto hazitakosa kuwepo. Lakini nategemesa sana sana kwamba suala la dawa halitokuwa tatizo kuanzia mwakani.

Suala jengine Mhe. Spika, la mama kutoleshwa fedha. Mhe. Naibu wangu alilisema na mimi napenda niliseme, na suala hili nikilisema nalisema kwa *motion* na nadhani mwaka jana pia nililisema hapa. Mhe. Spika, kwamba pamoja na jeuri yako ya kuwa wewe ni Spika, wewe umezaliwa na mama, pamoja na jeuri yangu kuwa Waziri mimi nimezaliwa na mama pamoja na jeuri zetu sote hapa hakuna asiyezaliwa na mama awe mwanamke awe mwanamme.

Kwa hivyo, hakuna sababu ya kuona mama wa mwenzetu anayeleta kiumbe chengine akazalilishwe atoleshwe fedha, samahani Mhe. Spika sina lugha nyengine mtanisamehe kwa sababu huwa nataka nifahamike, unapokuwa mama kama mjamzito kuzaa ana tumbo kabeba miezi tisa baba huna habari unapiga usingizi ni kazi aliyoichukua ya kuumiza anakuja kwenye *labour room* anazaa unamwambia atoe fedha, maana yake ukirudi usiende kulala na mumeo tena ndio maana yake.

Sasa ni kitu ambacho hatukipendi wala hakiniridhishi mimi na wala mwengine yoyote. Lakini tunapofika katika hali ya kwamba hakuna tumwache afe akose mtoto. Kwa hivyo daktari anasema chukua fedha kanunue kitu fulani, kinakwenda kununuliwa ili anusurike na yote haya yanatokea kwa sababu ya ukosefu huu wa dawa, hata hao wafanyakazi wetu wanaopata nafasi kumwambia lete pesa ni kwa sababu ya upungufu zinapokuwa dawa zipo za kutosha hana sababu ya kuuza dawa, si ajabu Mwenyezi Mungu nisamehe kwamba wengine labda wanafurahia ziwe hazipo ili wapate biashara.

Lakini sisi kama wizara, sisi kama Serikali, sisi kama wasimamizi tunajitahidi suala la kina mama lisitokee kudhalilishwa. Nilisema mwaka jana ilikuwa Mhe. Rais tuko Kizimkazi tunafungua kituo cha kina mama akanambia Mhe. Waziri husemi nikamwambia Mheshimiwa mimi sina cha kusema, watasema watu wa kijiji, akanambia sema tu niliposema nilisema kama hivi ninavyokwambia mimi: Nikamwambia Mhe. Rais umeona hawa kina mama hapa wote hao ni matokeo ya kwamba wao ndio waliotuzaa. Kuna bibi mmoja alikuja na mtoto, nikamwambia umemuona bibi yule, yule yuko kazini tangu siku ya kwanza alipochukua mimba mpaka leo analea kaja kukusikiliza huku ana kazi mkononi. Nikamuuliza Mhe. Rais tunawafanyia hawa wajibu wetu? Mhe. Rais akatikisa kichwa siku ya pili yalipokuja majumuisho akasema kuanzia leo hakuna ruhusa ya mama kulipa.

Kwa hivyo, tusilaumiwe kufikiri tunalifurahia, mimi silifurahii na wala silipendi, mimi nimezaliwa huko kichochoroni huko chini ya migomba hakuna mkunga, hakuna dawa ya *panadol,* hakuna chochote, ni matokeo yaliyokuwa yametokea akaambiwa kamuite mama yake Juma anataka kujifungua nipo hapa leo. Hilo ndilo linalonipa mimi kwamba nina wajibu wa kuwahudumia kina mama. Kwa hivyo, ndugu zangu hatufurahii hata kidogo wala hatupendi, na mimi nashukuru kwamba hili mnalieleza kila mara ili tuweze kulitekeleza hilo.

Mhe. Spika, upungufu wa wafanyakazi, tangu nimeanza wizara hii nikija kutoa majumuisho nasema bado nina upungufu wa wafanyakazi. Mambo mawili makubwa nasema nimejitahidi pamoja na wenzangu hii hapa *summary*

ya *man power planning* yetu yote tunajua hata kituo gani kina upungufu wa nani.

Tunajua nani anastahiki kuwa na mtu gani na katika Wizara za Serikali kama nakumbuka Mhe. Waziri alisema sisi ni wizara ya kwanza kuwa na Kamati inaitwa *deployment committee* nimemkabidhi Mhe. Naibu wangu anahakikisha kabla ya wale watoto wa Mbweni hawajatoka au wameshamaliza anawaita Wakurungezi wote, wakuu wa vituo vyote Unguja na Pemba wanasema bwana tulichonacho hiki, wewe unahitaji nini mimi sina *pharmacy*, wewe unahitaji nini mie sina *laboratory*, wanagawana wakimaliza kila mmoja anajua wakinamaliza kila mmoja anajua na Mhe. Naibu wangu namshukuru kwa hilo hana mas-hara.

Kuna mmoja mara moja alimchezea baada ya kugawana wafanyakazi akaenda akafanya alivyotaka, alichapa barua na akamfukuza kwenye Kamati kwa sababu tunataka tufanye kazi kitaalamu na tupunguze matatizo. Kwa hivyo, suala la kusema kwamba Wapemba hawapelekwi au Wapemba hawapewi hamna, sisi tunagawa wafanyakazi.

Hivi sasa ningekuwa na muda ningesoma hapa hasa *summary* ya jinsi *distribution* ilivyokuwa. *Clinical officer* Pemba 28 Unguja 35, *PHND* wote tunahitaji Pemba na *Nursing general* 34 Pemba Unguja 26 *the full list*, lakini bado upungufu wa wafanyakazi haujamalizika, wanaotoka kule Mbweni hawazidi 300 kwa mwaka si wengi kwa kutosheleza.

Sasa kinachohitakija nini? Nakuja lile jengine la mishahara ya daktari na maposho. Kuna *system* inaitwa *retention scheme*. Vipi hawa tulionao ili wasiondoke Mhe. Spika, *maneno matamu yanamtoa nyoka pangoni* au siyo! Na sisi tunajua hapa kwamba unapofanyiwa wema unashukuru, unafurahia na unahadithia. Sasa katika masuala ya wafanyakazi retention *scheme* maana yake uwaendeleze wawepo kwa hivyo uwalipe mishahara mizuri uwape haki zao uwatambue na shida zao, na kwa sababu nimesomea mambo ya *Human Resource* Mhe. Spika, binaadamu yoyote iwe mimi, uwe wewe au yoyote ana sifa mbili za kibinaadamu ana *hard* na *soft*. *Hard* ndio hii hapa nimesimama nafanya kazi kutegemea mwisho wa mwezi nigaiwe pesa nile na watoto wangu.

Lakini *soft* leo umeamkaje yule mama yako anayeumwa hajambo Bi Mkubwa mbona leo hukufurahi ile kuitambua ile ina tofauti kubwa. Sasa hawa madaktari wanafanya kazi katika hali ngumu sana, dawa hakuna cha kupimia hana masaa yamefika mshahara hakuna mara nyengine katika kwake cha kukiacha hakuna kitu. Lazima tuwathamini, tuwatambue, tuwape haki zao na haki hizi hawana haja ya kuomba ndio kazi udaktari yenyewe ndio sifa zake.

Juzi nilikwenda kufunga mafunzo ya wanafunzi Mhe. Spika Mbweni wale waliomaliza. Nikawaambia ndugu zangu mie ni mwalimu, kazi yangu ni mwalimu hata kina Mhe. Ismail Jussa Ladhu Mhe. Assa Othman Hamad hawa wote wanafunzi wangu nashukuru *alhamdulillah*. Lakini hebu nawauliza na Mhe. Waziri Ali Juma Shamuhuna yuko hapa mimi sikumbuki mwalimu akaanza kazi akasomesha akapata *promotion* ya kuwa *director* akabaki mwalimu akajenga nyumba sikumbuki, sijui kama nimeeleweka ukibaki ualimu na chaki mpaka ukastaafu hata kibanda kinakushinda.

Lakini sifa ya ualimu ndio hii mwalimu shkamoo Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi yule pale, sasa hivi katoka nje nikamwambia aah bi mkubwa vipi akanambia shukurani ya walimu hii ana kikaratasi cha pesa.Nikamwabia kuwa haya ni malipo ya ualimu. Daktari furaha yake amkute mgonjwa kapoa hajali uchafu, hajali wakati, ndio kazi yenyewe inavyotaka. Sasa kama kila kitu utakimbilia fedha usichague udaktari, lakini haina maana usipate yale anayokulazimisha maana polisi kama hana sare ni raia. Sasa daktari kama hana koti hana ile ya kupimia kwa hiyo Mheshimiwa *retention scheme* lazima ni muhimu.

Isipokuwa tofauti yangu mimi natafautiana na Waheshimiwa kwamba hatuwezi kutafautiana kwa mishahara na wenzetu wa Bara. Maana kama kushindana kishahara changu mimi na Waziri wa Bara ni kikia cha mbuzi na hutoa mfano wa mkia wa mbuzi kwa kusudi watu waone kwamba kudura ya Mungu tu, maana mkia wa mbuzi hauzidi ni stara ya mbuzi wala hamuudhi lakini ndio Mungu kampa. Sasa tusilinganishe kiasi hicho, tulinganishe kwa hali ya uwezo wetu wa uchumi na kwamba tuwape madaktari haki zao.

Sasa suala la *scheme of service* mimi sijui Mhe. Haji Omar Kheri hayupo pale. Lakini nilivyoambiwa inaanza mwaka huu. Lakini suala la motisha hasa zile za *risk allowance* katibu wangu kanipa tayari kwamba Mhe. Haji Omar Kheri ameshajibu kwa *risk allowance* wataanza kupata wale wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu kuanzia mwaka huu.

Barua imeshakuja na kitu ambacho pia miaka miwili ndicho tunakiendea mbio hakikuwa rahisi kwa sababu miaka miwili tunakiendea mbio hakikuwa rahisi kwa sababu kina- *raise* Bajeti ya Wizara ya Afya na vile vile katika jumla ya matumizi. Nilitaka hilo nilieleze kwamba si kwamba masuala haya tumeyadharau.

Kwa hivyo, nimehakikisha *call allowances* na yote yanayohusika yanaingia hapa. Na naomba nikubali kwa wale wanaotudai tutaendelea kulipa, lakini *of course* kuna tofauti baina ya madaktari, *call allowance* na ma-*nurse* kulipwa *over time* nadhani Mhe. Naibu wangu amelieleza vizuri.

Suala la kutizamwa wagonjwa lilisemwa sana, nalo hivyo hivyo tulipokwenda bango kitita nikamwambia Mhe. Rais dunia nzima niliyotembea kila hospitali askari nimeikuta ina askari wake kwa kulinda usalama wa wagonjwa na usalama kwa wafanyakazi.

Lakini vile vile kwa usalama wa hospitali yenyewe. Waheshimiwa Wajumbe Mnazi Mmoja tulifanya mazoea kukawa ni kitu cha kawaida ikawa hata mama ntilie wako pale chini ya mkungu wanauza pale na taarifa za kuthibitisha hawa vijana masikini mambo yao yalivyokwenda vibaya akilazwa mmoja pale wodi wanaingia wengine na bangi inavutwa mle mle, wengine na unga wanavuta mle mle wewe unaona mgonjwa au kijana, wafanyakazi wetu wanaibiwa simu zao, kanga pale msikitini kulikuwa na *pair* kama 50 zilimetolewa sadaka kwa watu wanaokuja kusali, zote zimeibiwa. Nikamwambia Mhe. Rais tunahitaji kuchukua hatua, kwa masihara akaniambia Mhe. Waziri kama unaweza kuanzisha kikosi anzisha. Kwa hivyo, tulipata ruhusa, tuliwaeleza wakubwa ili kuilinda hospitali, ilikuwa vibaya jamani.

Hivi sasa sio kubaya kule ndani, tatizo lililozaliwa la kwamba wale wanaosubiri kutaka kuwaona wagonjwa wao, sio jambo la kufurahia wanakaa pale nje Mhe. Salmin Awadh alisema kwamba tumeondoa hatari ndani tumeweka nje. Lakini tumefanya *effort* kwa miaka miwili, hivi sasa turuhusiwe kujenga kijumba pale kwenye ile bustani, tena ingekuwa ni starehe kabisa. Kungejengwa kijumba pale tukaunga *cordon* hata ya juu ya lile jengo, nakumbuka kuna *saleable* iliyozunguka, ukakijenga kijengo pale watu wanaingia kwenye ki- *restaurant*, anapotaka kupinda kwenda hospitali anapanda ngazi anaingia kwenye jengo lile anateremka kwa usalama wa barabara, tukashauri hilo. Lakini sisi sio taasisi ya Mji Mkongwe, tukienda kwenye taasisi ya Mji Mkongwe, sisi sio taasisi ya Baraza la Mji, tukienda Baraza la Mji, tukaambiwa hapana hii ni njia kubwa ya kwenda Ikulu ni lazima mpate ruhusa Ikulu, tukaenda Ikulu.

Mhe. Spika, Ikulu wakakubali, Mji Mkongwe wakakubali. Nasikitika Mhe. Mwinyihaji Baraza la Mji wametukatalia, lakini hadi sasa tunaendelea ku- *negotiate* ili tuone jambo hili linapatikana. Ramani tayari tena wala halikuhitaji fedha za serikali, kuna wafadhili wamekubali kabisa kujitolea kutujengea kibanda hicho, ili watu wetu na jamaa zetu wakiwemo jamaa zangu wanaotoka Kaskazini na Kusini, anatoka kuja kumtizama mgonjwa halafu hawahi kurudi kwenda shamba kwa uwezo wa nauli basi angekaa pale akasubiri saa 10:00 ikafika akamtizama mgonjwa wake akaenda zake. Kwa hivyo, nalo ni suala lililoanza kwa njia hiyo, lakini kwa vyovyote vile kidogo ukiingia hospitali kuwe na salama.

Mhe. Spika, bajeti. Kitu nilichofurahi kwenye bajeti hii kwamba nimeweza kuziweka takwimu ili Wajumbe wakaweza kuzitafsiri, kwamba mara nyingi tunapoambiwa mambo huwa hatufanyi, huwa tunaonekana labda ni kwa sababu ya uzembe wetu. Hii ndio hali halisi ya mapato tulivyokuwa tumepata. Sasa kitu cha kwanza ningeomba kufanya masahihisho ile hoja ya Mhe. Ismail Jussa ya ile *table* nambari 17 sijui, labda pale ni 18 ni *topographic mistake.* Lakini ukifungua ukurasa wa 4 nilipokuwa nafanya *summary* ile 26.6 imejitokeza. kwa hivyo, nataka uniambie.

Sasa bajeti hii maana yake nini? Wengine waliitizama Pemba *v/s* Unguja, wengine wakaitizama jinsi *cash* ilivyo-*flow.* Sisi tulikuwa tunafikisha maombi yetu kwa serikali, tunafikisha wizara ya fedha na wizara ya fedha nadhani wana Kamati inaitwa *ceiling committee.* Wanatizama *overall picture* yote halafu wanatupa wanachotupa tunarudi tunatekeleza. Humu ndani nimeeleza mambo mengi tuliyoweza kutekeleza, tumeweza kutekeleza kwa kile kichache tulichopata na tumeweza kutekeleza kwa zile fedha tunazopata misaada kutoka nje.

Sasa hiki kilikuwa maisha yote hakinipi raha, nifanye nini ndugu zangu nimeshakwenda mara mbili kwa Rais kumueleza kwa *memo* kwamba Mhe. Rais hali ni hii, akaniambia unasemaje? Nikamuambia nitakuletea waraka. Nikapeleka waraka wa kwanza jinsi ya ku-*go about this problem*, wakauzingatia wakaturejesha kutupa kazi tena, tumepeleka waraka wa pili umezingatiwa, tumepewa kazi tena. Hivi ninavyokwambia tunahitajiwa kulikuwa kuna kikao Jumamosi ijayo niende na nyaraka mbili juu ya ku-s*olve problem* hii. Tupeleke waraka vipi tutaifanya Mnazi Mmoja iwe *referral* kwa maana ya *referral*, na tunahitaji nini na marekebisho gani yafanywe. Hata lile jumba labda ni la karne ya 17 sote tulikuwa hatujazaliwa, pamoja na Spika wangu na liko vile linahitaji *overhaul*. Tumempata mtaalamu kutoka *BADEA*, ata-*finance* kufanya *cost* na *feasibility study* lirekebishwe vipi. Kwa hivyo, yale madirisha mabovu Mhe. Jaku Hashim Ayoub yote tunahitaji lile. Lakini linahitaji fedha nyingi.

Ndugu zangu kama tunataka Hospitali ya Mnazi Mmoja iwe *referral in the real things.* Nakuambieni nafanya hilo zoezi kila kitengo kiwe *fully* kama kinavyotakiwa sio chini ya bilioni 35. Watu wasiitizame ile kama labda ni kitaasisi kidogo, katika mfumo hasa wa taasisi wa *referral*, maana yake dawa iwepo, ukitaka *X-Ray* iwepo, ukitaka *CTN* sijui iwepo, ukitaka kwenda *laboratory* tayari. Isiwe kwamba aah! Leo hakuna zimekwisha, aah! Sijui huyo mama kenda mazikoni. Hiyo itakuwa sio *referral*, Kwa hivyo nilitakiwa kupeleka huo waraka na tunategemea kupata waraka. Hilo la kwanza.

La pili vipi tutaisaidia serikali katika uwezo wake mchache kuisaidia kupata njia nyengine za kupata fedha, hiyo ndio kazi ya pili niliyopewa yaani inaitwa *alternative health finance.* Tumepeleka waraka wa kwanza tumerudi, tumepewa kazi na tumewatafuta wataalamu hivi sasa wanaishughulikia kazi hiyo, tutakapopeleka waraka wa pili tutajua sasa kipi kichangiwe na wananchi, kipi kitolewe na serikali, kipi kitolewe na *donors* na kipi kitolewe na *private sector*. Lakini mambo haya yalikuwa hayapo, sasa ndugu zangu tusitegemee labda leo au kesho yatakuwa, nipeni nafasi pengine baada ya mwaka mmoja au miwili, mwaka mmoja uliobaki, nategemea miaka miwili hii ikimaliza tukitoka mimi na mwenzangu angalau tuache *legacy*, kitu gani tumeweza kuisaidia nchi hii na serikali katika kurekebisha mambo haya. Tupeni muda.

Sasa ninachowaomba wananchi na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, sio suala la kusema muirejeshe bajeti. Mukiirejesha bajeti maana yake hivyo vibaya tulivyo basi vizidi kuwa vibaya ndio maana yake. Kinachohitajika ni kushirikiana tukasaidiana, tumeziona *concern* zenu tumezipokea, serikali imesikia, kwa bahati nzuri Kaimu Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hapa amesikia, vitabu vimesoma kuwa ni kipaumbele, *commitment* zimeanza na zinaonekana kufahamika, imetuchukua muda sana kushawishi kueleweka. Natamani ningekuwa naweza kukuelezeni yote hapa ninachukua kama hivi ninavyochukua muda kuwashawishini, ninashawishi hasa kwa hoja ili nieleweke kwamba jamani tunaposema afya bure maana yake hii.

Mhe. Spika, Tumefanya majaribio, mahitaji ya kuhitaji *primary health*, hivyo vituo vilivyokuwepo shamba tu ni 134, ili vifanye kazi vizuri na kuwe hakuna tatizo la dawa, hakuna tatizo la wafanyakazi na hakuna tatizo la umeme, basi tunahitaji 12.6 bilioni. Katika 12.6 bilioni, 6 bilioni ni mishahara na maposho na mambo ya nyumba ili hao watu wawe wanafanya kazi moja kwa moja. Hujatia hospitali za *district*, hujatia hospitali za vijiji na hujatia hospitali ya Mnazi Mmoja.

Kwa hivyo, *issue* sio finyu, *issue* ni *wider* kuliko vile. Nawaambia Wajumbe wa BLW kwamba hivi tulivyo sasa kwa *primary health* tunataka 12.6, hatujaingia *secondary*, hatujaingia *tertiary. Project* kubwa inakuja ya kubadilisha ambayo inahitaji si chini ya 17 bilioni. Kunakuja *neurological unit* itajengwa pale ya wale watu wenye matatizo ya mgongo, kunakuja *ward* ya kinamama na watoto, kunakuja hospitali ya Mkoani Pemba, tunaimarisha hospitali ziende wilaya. Sasa litizameni hilo juu ya jamvi limekukalia hapo, walimu, wafanyakazi, madaktari, *administration* yake.

Kwa hivyo, ninachotaka kusema ni kwamba tunahitaji kushirikiana ili bajeti hii iweze kutekelezeka katika angalau hiki tunachopewa na *commitment* ya serikali pamoja na Waziri wa fedha mara hii kasema hata lazima tutimize wajibu wetu. Mhe. Spika, haya yalikuwa ni katika mambo makubwa ambayo nilitaka niyapeleleze yamekwenda *across the board.* Sasa mule mwengine ambamo nitakuwa sikumueleza mtu mmoja mmoja nilikuwa na maana kwamba hayo yote yatakuwa nimeyaeleza kwa pamoja.

Mhe. Spika, baada ya hapo kuna mambo ya mmoja mmoja ambayo nadhani pengine nitasema hili limeshasemwa na Dk. Sira nitakuwa sipati kupoteza muda zaidi. Ilikuwa Kamati ya Ustawi wa Jamii, walieleza baadhi ya mambo kama ujenzi wa vituo vile vya Wesha havijawa tayari Mzambarautakau sijui Mzambarauni kule hii yote sasa *tender* tayari, vyengine vimeshaanza kujengwa. Kivunge nina hakika mwisho wa mwezi Julai ukimalizika nyumba zote zile za Kivunge zitakuwa zimeshajengwa na *theatre* inaendelea kujengwa. Na Mhe. Kazija alitaka *gate* pale. *Gate* wameshakabidhiwa wale watu wa RANZI ili waweze kulijenga pale na baada ya muda itakuwa mbwa tena hawatoingia kwenye hospitali ile.

Vile vile kulikuwa na suala la Mfuko wa Basket Fund, utaratibu wake ulikuwa haueleweki. Ule utaratibu haujabadilika isipokuwa hivi sasa inabidi uingie kwenye serikali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliyasema mengi mengine yameshajibiwa na Naibu Waziri wangu, hasa mambo ya saa 24 ya *X-Ray* yote ameshayaeleza. Jengo la macho bovu, ni kweli bovu, lakini sababu yake sio ile sababu iliyotolewa na Mhe. Hija Hassan. Mhe. Hija Hassan yeye alikuwa akisema kwamba kulikuwa kuna milioni 30 zimechukuliwa nikaeleza hapa na *document* tunayo, kwamba mradi ule ulikuwa wa milioni 113 na zote zililipwa, 108 zililipwa na wizara, zikabaki milioni 7 ikabidi Mhe. Aman Karume amlipe Fatuma Kara kutimiza ile *project*. Kwa hivyo, hakukuwa na milioni 30 zilizochukuliwa na mradi ule ulikuwa ni kuezeka bati na yeye Fatuma Kara alipokuwa anaeleza hiyo *tender* alipopewa na *consultant*, akasema hapa sio zaidi ya bati na hilo jengo lenyewe kwa sababu wewe ni mtu wa Baraza la Mji Mkongwe, akashauri hivyo, lakini kulikuwa hakuna fedha.

Hivi sasa watu wale wamehamishwa tumeshalieleza Baraza la Mji, ripoti imeshaandikwa, tumeshashauriwa, ma-*engineer* wetu wa wizara wameshafanya, ma-*engineer* wa Baraza la Mji wameshakwenda, tutaliombea fedha katika njia ya misaada. Lakini kuweka historia jengo lile sio vizuri kulivunja, kwa sababu lile na hili kubwa yamejengwa karibu wakati mmoja.

Kuhusu mambo ya *risk allowance* yameshaelezwa, chakula cha wagonjwa ni kutokana na ukosefu wa fedha. Fedha tulizopata zilikuwa haziruhusu, *emergency room* imeshaelezwa. Suala la Rahaleo limeshaelezwa. Liliulizwa suala la kampuni gani iliyopewa mkataba wa kulinda. Kampuni hiyo inaitwa *Samu Security* ndio inayofanya kazi pale kulinda watu wetu wanaoingia na kutoka pale.

Vile vile kuhusu wanafunzi kuachiwa wagonjwa nimeshaeleza na limetolewa ufafanuzi. Kulikuwa na masuala ya chanjo, sisi dawa tunachangia, tunanunua gesi na mafuta. Mhe. Jaku Hashim Ayoub alisema suala moja Mhe. Spika, nalo naomba nipate nafasi ya kulieleza, ni kuhusu eti tunawadharau wauguzi.

Mhe. Spika, hatuwadharau wauguzi, niko pale kwa miaka miwili wamekuwa wakinialika kufungua siku yao ya wauguzi. Sasa ile naambiwa ilitokea dharau kulikuwa kuna matatizo ya mawasiliano, mimi kama waziri nilikuwa lazima niende Nungwi, alikuwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais anafungua bomba la maji Nungwi na nilikuwa nimeshapewa barua. Nilitegemea watendaji watakwenda pale na kwa bi Asha. Aliyeandika barua kumualika yule ni Katibu Mkuu wangu.

Mhe. Naibu Waziri yeye alikuwa amekwenda katika mambo ya chama chao Makunduchi. Sasa asubuhi tukitegemea waliobaki watakwenda, kwa bahati mbaya yakakosekana mawasiliano, sio kwa sababu ya kusudi. Lakini kitu kimoja ambacho nataka nikiseme na hiki nakisema kwa uwazi wala sina nia mbaya. Ni kwamba jambo likishatokea Wizara ya Afya, hee! Inakuwa kama nguru, akichomwa ananuka! Ilipotokea *issue* ile, ikawa redio, TV, mazungumzo baada ya habari, magazeti ya Zanzibar Leo, ee bwana ee mama Asha kadharauliwa. Eeh! Jamani! Hatukuwa na nia ya kumdharau mama Asha. Baada ya kuona limetokea lile na ninalisema watu wote wananisikia nchi nzima. Tukaenda tukamuomba radhi *physically* Katibu Mkuu wangu akaenda, mama tusamehe, kulikuwa na matatizo ya mawasiliano ndio maana likatokea. Nikamwambia bado Dk. Jidawi andika barua. Dk. Jidawi akaandika barua, mama tunakuomba radhi. Bi Asha akaandika barua nimewasamehe. Sasa ubinaadamu gani mnaotaka tufanye jamani, kutuandika magazetini kama tumeua Mungu, hivi Mungu hufa. *Astaghfirullah* Mwenyezi Mungu tusamehe. Mara nyengine yanakuwa *over done* Mhe. Spika.

Lakini likatokea la Mpendae. Yuko wapi Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa hayupo. Alikwenda Rais tukawa nako hatupo. Nalo sio kosa letu, lakini mimi sipendi kuwasema viongozi *public*, ilikuwa ni makosa ya mawasiliano baina ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Wizara. Asubuhi nilikuwepo Ofisi ya Mkoa, Mhe. Rais anafungua ziara ya Mkoa wa Mjini, nikaitizama ratiba, wizarani mule simo wala hamna *activity* yoyote inayohusu

Wizara ya Afya, tukashirikiana pale tukateremka. Nateremka chini akatokea ofisa mmoja wa Ikulu, akaniambia aah! Mheshimiwa tunategemea kwenda Mpendae. Nikawaambia aah! Jamani mnanionea na mimi Waziri, karatasi yenu hii hapa na mimi simo, basi angalau iwe kesho. Yaliyotokea saa 9:15 akapigiwa simu Dk. Malik, niko wazi kabisa. Dk. Malik akasema Mheshimiwa saa 9:30 Rais anakwenda Mpendae. Nikamwambia Dk. Malik usiende, usije ukafa njiani hapo ikawa sababu unamkimbilia Rais. Ni mtu gani saa 9:15 anapigiwa simu ili saa 9:30 afike Mpendae, nikamwambia tungoje matokeo. Lakini wakati huo Naibu Waziri wangu nilimuagiza tangu mchana hebu kasikilize hiyo ziara ipo, akamtuma ofisi ya wilaya akenda kule, alipokaa kule mpaka saa 7:00 bado, lilipotokea bahati mbaya ikawa hakuna mawasiliano.

Mhe. Spika, nilikwenda *physically* mwenyewe, nikamwambia Rais nataka kukuona, akaniambia tuonane baada ya BLM. Nikamwambia nimekuja kukuomba radhi Mhe. Rais lililotokea ni a, b, c, na d. Lakini sisi washamba ukishafanya kosa ambalo hukukusudia, kule kufanya kosa ni adabu. Mhe. Rais alitikisa kichwa akaniambia Mhe. Juma limekwisha. Uungwana gani zaidi ningefanya kwa kuandikwa magazetini. Wakati mimi naandikwa magazetini tuko Nungwi, Mkuu wa Mkoa hakwenda, Mkuu wa Wilaya hakwenda na Sheha kakimbia, haikuandikwa wala haikusemwa. Tafadhalini mambo haya yasiwe yanapigiwa pampu, yasemwe vile yanavyostahiki! *(Makofi).*

Mhe. Spika, hili nimelisema kwa sababu limeelezwa na nimepata nafasi ya kulieleza. Suala lililokuwa linaelezwa zaidi na ambalo limeelezwa na *FBA*, sisi tunashughulikia wenye *certificate*, wale wauza madawa wa mitaani na wengine wa kienyeji wale wanashughulikiwa na Baraza la Mji, sisi wale waliokuwa *registered*.

Mhe. Spika, *ICU* nayo imetajwa, tulijitahidi huko nyuma *ICU* itengenezwe, ilitengenezwa kwa kile tulichoweza kupata, tulitegemea tungekuwa na *monitor* 6, lakini tumepata 3 zipo pale zikiharibika tunatengeneza. Lakini jana nilisema hapa kwamba *ICU* itajengwa yote na Serikali ya China kama vile ilivyoahidiwa na itajengwa kuanzia mwaka huu, pengine mpaka mwezi wa Disemba walivyotuambia wale ma-*engineer* kwamba itakuwa imemalizika. Itarekebishwa ile *flow* yote na itapangwa upya na kutakuwa nadhani kama sikosei vitanda 8 katika *ICU, modern* na kila kitu, na ramani juzi tumeziona tumesahihisha kamati ya viongozi pale wizarani na mabingwa kutoka China mibuku yote ile ilikuja pamoja na ile ya Pemba.

Vifaa vya Bandarini nadhani vimeelezwa, nilikuwa namtafuta Mhe. Makame Mshimba ambaye yeye alitizama fedha za likizo akasema 25,000 zimetoka

mpaka 33,000. Lakini Mhe. Makame Mshimba kulikuwa na hoja mbili. Mhe. Mshimba hoja yake kubwa ilikuwa ni vifaa vya *cancer*. Alilisema katika bajeti iliyopita, alilisema katika maswali na alilisema juzi. Tunamshukuru kwa *consistence* ya kushika hoja hii. Ukweli ukoje kwa vifaa hivi? Vilikuja *laboratory* ile inatengenezwa, vikaenda kuwekwa Bweni, hakuna kilichofunguliwa yakawekwa maboksi kwa kuwa kila kitu kiko sawa itakapomalizika *laboratory* itakuja kufunguliwa. Ilipomaliza *laboratory* ilipofunguliwa kukawa na vitu vimepungua. Kuna vitu vimekaa muda mrefu vimefanya mchoro, wakawasiliana maofisa na yule aliyeagiza. Wakati huo *laboratory* imemaliza kujengwa, *guarantee time* imekwisha. Akasema mimi *guarantee time* imekwisha, lakini nitajaribu kuvitafuta, alitafuta ameshindwa.

Sasa Mhe. Mshimba ukweli ni kwamba tumekosea sawa na inawezekana tumezembea, lakini hatujamdanganya kiongozi yeyote kumpaka matope ya uso. Mhe. Makamu wa Rais tulimueleza wazi ilivyotokea na leo nalieleza wazi kwamba tumekosea na makosa maafisa wetu wanayo. Sasa kuna njia mbili Mhe. Mshimba, yule mwenye ushahidi aende kwa *DPP* ifunguliwe kesi ashitakiwe ofisa wetu yeyote anayehusika uje ushahidi, zipite taratibu za serikali. Vinginevyo hivi ninavyozungumza Rais ndiye aliyeniteua mimi na ndiye aliyemteua Katibu Mkuu na Wakurugenzi wetu, kama tunastahiki kutiwa adabu anasikia basi na amuondowe amlete mwengine. Lakini nadhani sio vizuri kwamba suala hili kila mara ikawa kama vile paukwa pakawa. Tumekosea, tunastahiki kutiwa adabu, na tutiwe adabu limalizike.

Mhe. Spika, kuhusu *Insulin*. *Insulin* nililieleza kwa urefu kwa maandishi Mhe. Spika, kama unakumbuka jinsi mambo yanavyokwenda. Mhe. Naibu Waziri wangu amejaribu kulieleza kwamba jamani tumegawana kazi. *Pharmacist* kazi yake ni kusimamia sera ya dawa na kuhakikisha dawa zipo. Daktari kazi yake kusema Juma Duni unaumwa na nini nenda kachukue dawa fulani. Ukichukua kazi ya kutibu ukaifanya ni kazi ya kutafuta dawa, tunachanganya mseto nililieleza. Moja ikaambiwa kwa nini daktari asishauriwe. Kwa hivyo, ina maana kila tukitaka kununua dawa tumuite daktari njoo unasemaje, hiyo haitakuwa tena *tender*.

Mhe. Spika, Nilisema hapa juzi kwamba jamani tunachoepuka asiwe daktari ni wakala wa dawa, akiwa daktari yuko kwenye *desk* na bado ni wakala wa dawa ni makosa. Nilisema kwamba Dk. Kaushak nilimuita, nikamuuliza akashindwa kujibu, nikamwambia anipe kwa maandishi akashindwa kujibu, akaleta kwa E-Mail hakutia saini, unapokuwa *document* hukutia saini maana yake hukuji-*commit*. Sasa Mhe. Mshimba ni kwamba yule Dk. Kaushak yeye mwenyewe, *I am sorry to say that*, yeye mwenyewe ni *interested part* katika ile dawa, sasa akishakuwa *interested* pale kusema itumike maana yake anaweza kukosa ule u-*urgent*, na kusema isitumike akanyamaza kimya.

Lakini jamani dawa ile inatumika kote, hizi hapa Mhe. Spika, naomba nikuwasilishie, hii hapa *Pharmacy and Poison Board Ministry of Medical Services Republic of Kenya.* Hii dawa imesajiliwa na inatumiwa Kenya, *Republic of Namibia* hii hapa inatumika Namibia, hizi hapa *Certificate* ya Dar es Salaam hizi hapa *registration* za dawa hiyo, tungefanya nini zaidi na ndio kazi ya wale wanaohusika.

Mhe. Spika, *WHO* sio dhamana wa *regulatory board*, *WHO* ni *advisor. Regulatory board* ya dawa ni zile bodi zilioko nchini, kwa hapa kwetu ni *ZFBA* na kwa Tanzania ni *TFBA* na kwa Kenya ni hii hapa. Hawa ndio wanaokuwa dhamana, jamani tumalize *issue* hii tufanye kazi nyengine. Mhe. Spika, nadhani nimefahamika. *(Makofi).*

Mhe. Spika, mambo ya *risk allowance* nadhani yamesemwa, kuhusu unga mbovu amejibu Mhe. Fatma. Bwana Suleiman Hemed amesaidiwa na Dk. Sira. Mhe. Asaa Othman umesaidiwa na Dk. Sira. Mhe. Abdalla Juma ameeleza ambayo mengi ni wale wagonjwa wa nje, fedha nyingi. Tunajitahidi, tulipokwenda serikalini ndio tumeambiwa, siku tutaeleza ni mahitaji gani ya kuifanya Hospitali ya Mnazi Mmoja iwe ya rufaa, mambo mengine yatapungua tutakuwa hatuna suala la kupeleka wagonjwa nje nalo litapungua.

Kuhusu ile *data* pale, maskini tumekosea kidogo. Ile 335 ilikuwa ni ya mwaka wa nyuma, ile halisi ilikuwa ni 492 nadhani, lakini hayo ni masahihisho tu.

Kuhusu Mhe. Ismail Jussa Ladhu, baadhi ya mambo yameelezwa na Mhe. Sira. Migao ya fedha kweli ni michache, tumeeleza lakini hali halisi na nilieleza kwa jumla kwamba tumepata hiyo hali ya mambo kubadilika. Suala la Katibu Mkuu wetu nadhani Mhe. Naibu Waziri Dk. Sira amelieleza.

Mhe. Spika, sidhani kama ni vizuri tukiwa humu kumtaja mtu kwa jina moja kwa moja mpaka uwe na ushahidi, pengine Mhe. Ismail Jussa Ladhu anao ushahidi kuhusu hizi *claim* anazozisema kuhusu Dk. Jidawi. Lakini kitu kimoja tu nilitaka kumueleza Mhe. Jussa, ile mishahara na marupurupu ya wafanyakazi yanafanywa na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na wizara ya utumishi inawezekana kwamba walipeleka waraka katika kamati ya makatibu wakuu, kwa bahati mbaya mimi sifiki katika kamati ya makatibu wakuu na wala sijapata taarifa hiyo, kwamba inawezekana Dk. Jidawi kazuwia, sidhani na siamini hivyo. Pengine katika ile hamu ya Mhe. Ismail Jussa ya watu kuona hawapati maslahi yao basi wanaweza kuja na taarifa zozote wakakueleza. Lakini kama uliweza kupata barua mpaka kwenye vyombo vya ulinzi kwa watu kudai haki zao, basi

inawezekana vile vile umepata taarifa hizi. Basi kama zipo labda utusaidie, kwa sababu ni suala la kibinadamu, lakini mimi sina tatizo na Dk. Jidawi kuhusu hili kwamba linaweza kutokea.

Suala la uzazi wa wanawake lilishazungumzwa, ile *figure* niliyokuambia imekosewa ni ukurasa wa 4, kifungu 106 imeonesha ile 26. Kwa hivyo, ile ilikuwa ni *technical error*. Kuhusu kulipishwa tumeshaeleza. *Oxygen* hakuna Hospitali ya Mnazi Mmoja, ni kweli tangu juzi ilikuwa hakuna, lakini ndio tunamalizia bajeti hapa Katibu Mkuu wangu siku aliyonijia na Mkurugenzi, ilikuwa ni juzi. Walinijia ofisini, wakaniambia Mheshimiwa tuna hali hii hatuna fedha. Nikamwambia toka nenda wizara ya fedha, akawakuta wakubwa wote hawapo; Waziri hayupo, Katibu Mkuu hayupo na yule Omar hayupo, kuna Naibu Katibu Mkuu alikuwepo Dar es Salaam akawasiliana naye wakafahamiana, siku ya pili akaenda akapata fedha, nadhani tatizo hilo limekwisha.

Mhe. Spika, tatizo lililokuwepo ni moja siku hizi kwamba zile *account* zote ziko pale wizara ya fedha, sio zamani. Zamani zilikuwa zinatiwa fedha kwenye *account*, siku hizi utaratibu wote ni lazima umalize kwenye makaratasi mwisho izuiwe wizara ya fedha. Kwa hivyo, inaweza ikachukua siku mbili mpaka tatu na siku ile iliyokuwa imetokea ilikuwa ni siku ya Ijumaa, nina hakika jana labda Katibu Mkuu ataweza kulisema, lakini kasema limeshatatuliwa. Inatokea hiyo mara nyengine na kwa sababu huu ni mwaka mpya.

Mhe. Spika, kuhusu wagonjwa wa nje. Nalo hili napenda nilieleza na kuna *data* pale ni muhimu bora niliseme hili Mhe. Spika, unistahamilie. Unapotizama zile asilimia kama mtafungua kiambatanisho 18 kinasema, kwamba asilimia 235 kwamba walitengewa asilimia 435, wakapewa bilioni 1,093,000,000 asilimia ni 251. Hii ilitulazimisha kwa sababu lile fungu la 435 ni mwezi mmoja tu au miwili imekwisha. Sasa wagonjwa wanaendelea kuja. Mhe. Spika, katika kitu ambacho kinanipa unyonge ni kwamba watu wanakuja wanaomba wapelekwe nje na uwezo si mkubwa na fedha hazitoshi, basi tunaishia kwenda Wizara ya Fedha. Mhe. Spika, tuko hali hii kwamba tunapata mashirikiano na Wizara ya Fedha, lakini haziwezi kutolewa fedha nje ya zile zilizomo kwenye bajeti ya Wizara ya Afya. Kwa hivyo, tunaambiwa kwamba bwana tutakupeni fedha ziada, lakini mujue kuwa fedha hizi ni sehemu ya bajeti yenu.

Hali hiyo, kwa kweli inatuathiri, lakini hakuna bei ya uhai Mhe. Spika, na wala sijawahi kusikia kwamba kuna bei ya maisha, kwa hiyo tunapewa na halafu vifungu vyetu vyengine inabidi tuhaulishe. Kutokana na hali hiyo, ina maana kifungu hichi kikaonekana kina *percentage* kubwa.

Lakini ukweli ni kwamba tulipangiwa iwepo 35 na wagonjwa hawa ni wa Unguja na Pemba na wala Pemba hawasafirishi wagonjwa. Kwa hivyo, kifungu hichi kinapoonekana labda cha Tiba cha Zanzibar ni kikubwa ni kutokana na sababu hiyo zaidi. Mhe. Spika, hilo nalo nilitaka lieleweke katika sura hiyo.

Mhe. Spika, suala ni kwamba kila tutakapopata *capacity* hapa ya kuweza kufanya hayo matibabu Hospitali ya Mnazi Mmoja basi hili litapungua. Mhe. Spika, kwa taarifa kuna mwekezaji mmoja anajaribu kutaka kujenga hospitali hapa, ili kuweza kutumia wataalamu wa Kikorea atawaleta hapa. Sasa hospitali hiyo itakapokwisha kwa lile ambalo itakuwa hatuliwezi pengine tunaweza kushirikiana tuka-*refer* kwa hospitali hiyo, lakini hospitali yenyewe bado haijesha, hivyo ndivyo tulivyo.

Vile vile Mhe. Kazija Khamis Kona aliuliza hivi Hospitali ya Mnazi Mmoja ni Hospitali ya Rufaa au si ya rufaa. Mhe. Spika, Hospitali ya Rufaa kwa hali ilivyo sasa, kwa sababu ni hospitali ya juu kuliko zote, lakini rufaa ukitoka kituo cha mwanzo, unapokwenda pale Kivunge basi pale ni rufaa kwa kituo kile.

Kwa mfano, kwa upande wa Pemba unapotoka Micheweni ukaja Wete, basi pale ni rufaa kwa kulingana na Micheweni, pia ukotoka Wete ukimleta Hospitali ya Mnazi Mmoja hii ni rufaa kwa Wete. Kwa hivyo, hii *level* ya rufaa inatoka kwenye daraja moja ya uwezo wa kutibu kwenda kwenye daraja nyengine. Sasa tunachotaka kufanya iwe Hospitali ya Mnazi Mmoja iwe ni Hospitali ya Rufaa ya kweli kama vile inavyostahiki kupelekwa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia Mhe. Mjumbe alizungumzia kuhusu suala la kwamba kuna mgonjwa anakuja anatizamwa na halafu anaambiwa hebu tukutane ng'ambo, yaani wale madaktari wetu pale wanakuwa wamekuja ku-*fish customers*. Mhe. Spika, inawezekana na wala sisemi kwamba halipo, inawezekana lipo.

Tatizo tunalolisema ndilo lile alilolisema Mhe. Naibu Waziri, kwamba ah! Yule mgonjwa anapopata matatizo hayo, basi awe anatuarifu, ili sisi tumueleze yule daktari wetu kwamba hapa si sokoni, isipokuwa hapa wewe umekuja kutibu, kwa hivyo tibu kwa mazingira ya hapa na kama huyo amekuja kwenye *Dispensary* yako basi mukutane ng'ambo. Sasa inawezekana lipo na wala hatukatai, lakini jamani tuelezeni na imekuwa kama vile watu wanakuja kufanya *shopping* na Mwenyezi Mungu atunusuru.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, jitahidi na muda.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, *Inshaallah*. Mhe. Abdalla Moh'd Ali alizungumzia kuhusu *compensation* za Pemba, kwamba wale watakaolipiwa je, imezingatiwa maeneo na kima cha fedha alicholipwa na kwamba je kiwanja atakachokwenda nunua kimezingatiwa. Kwa kweli mengine siyajui, lakini kwa hili viwanja watapewa bure wale wanaokuwa *compensative* na makisio yaliyofanywa hayakufanywa na watu wa kawaida, isipokuwa yamefanywa kitaalamu.

Mhe. Spika, wamekwenda watu wawili, yaani watu wa kwetu pamoja na watu wa Majenzi kwa mashirikiano amekwenda Katibu Mkuu wangu na Katibu Mkuu Fedha wameshirikiana. Kwa hivyo, ile orodha ya fedha tulizoziandika ni baada ya makisio hayo na tumeambiwa kwamba viwanja watapewa bure na Mkuu wa Wilaya.

Mhe. Spika, mambo mengine yameshajibiwa na yanajirudia na wala sina haja ya kuyaeleza. Vile vile suala la *PHL* nalo limeshaelezwa.

Pia kulikuwa na suala la mawasiliano ya malaria kwa simu. Kwa kweli ule ni mtandao uliopo zamani na unaotusaidia sana na jinsi ulivyomzuri nimewapa kazi watu wa Malaria, kwamba kwa nini hatuwezi kuutumia mtandao ule kwa kutumia kuwajua wazazi, ili mzazi akeshachukua mimba tu basi tupigiwe simu kwamba hapa Kijiji cha Kibeni kuna mama mjamzito hapa, basi tuanze kumfuata kuanzia mwezi wa kwanza mpaka ajifungue badala ya kumngojea mwezi wa 9 anakuja hana kitu. Kwa hivyo, ule mtindo ni mzuri sana na upo na unaendelea vizuri na utatusaidia sana katika kuendeleza harakati hizo.

Mhe. Mjumbe, aliuliza kuhusu suala la uchangiaji damu, kwamba vipi tumejiandaa vizuri wakati wafadhili watakapoondoka. Mhe. Spika, tumejiandaa vizuri na kuna vituo 34 vya *NCD*, ambavyo navyo tayari vimeshakaguliwa kuweza kusaidia shughuli hiyo.

Jengine ambalo nadhani limeulizwa na Mhe. Salma Mussa Bilali kuhusu mfanyakazi wa Wawi. Kwa kweli yule ambaye yupo tumempeleka sisi na mwengine alikuwa anakwenda kusaidia, lakini katika ugawaji wa wafanyakazi tunategemea kumpeleka mwengine, kwa sababu huduma kila zikiwa nzuri basi hilo linatupa nafuu na sisi.

Mhe. Nassor Salim Ali tayari ameshajibiwa kuhusu yule mgonjwa.

Mhe. Subeit Khamis Faki tunafurahi kwamba umefahamu juhudi zetu za kusaidia Hospitali ya Micheweni. Kwa kweli kuna *First Class Laboratory*, ambayo imejengwa na inahitaji wafanyakazi na tutaendelea kusaidiana kwa ajili ya kumpatia wafanyakazi.

Mkemia Mkuu Pemba ilizungumzwa kwamba hana kitu. Mhe. Spika, ukweli ni kwamba anazo shilingi milioni 132 na hawa kuanzia mwaka huu wanapata ruzuku. Kwa hivyo, unaweza kuona kwamba badala ya kugaiwa vile visenti wakaja kwa Katibu Mkuu, basi watakuwa wanapata fedha zao moja kwa moja.

Nikiendelea na majumuisho Mhe. Mussa Ali Hassan alizungumzia masuala mawili. Kwanza alisema kuhusu vituo vilivyoko Wilaya pamoja na Mkoa wa Kusini viko mbali mbali sana, kwa hivyo wagonjwa wa *HIV* wanapotaka kufuatilia mambo yao inabidi waende Makunduchi ni mbali, na kama inawezekana kingeongezwa chengine.

Mhe. Spika, hatukatai, lakini masharti ya kuongeza kituo, lazima kuwe na daktari, mfamasia, maabara, mshauri pamoja na chumba ambacho ni safi. Sasa mazingira ya vituo vile kwa sasa hayajaruhusu, basi hali hiyo itakaporuhusu sisi hatuna tabu kuongeza kituo hicho.

Lakini hasa aliyoishika na kuniambia atanizuilia bajeti ni yule daktari kuwa hakai kule kisiwani Uzi. Mhe. Spika, yule daktari bahati nzuri anayo namba ya simu yangu, asubuhi niko garini nakuta *message* na nikamuuliza wewe nani? Akaniambia mimi ni daktari wa hicho kisiwa na jana nimeambiwa kwamba silali kule, nikamwambia ndio kwa hiyo unanipa matatizo, akasema kweli Mhe. Waziri silali, kwa sababu kule kisiwani ikiwa nitalala si tatizo, lakini maana yake 24 *hours* niwe kwenye kazi na hiyo ndio dhamira.

Mhe. Spika, ile hali yenyewe sijui kama munaelewa, yaani hali yenyewe kama nikiwa nitakaa kule masaa yote 24, basi ule uwezo sina. Kwa hivyo, ninapokuwa ninakuja mjini na kurudi basi huwa ninajisaidia kwa mambo mengine. Mimi nilimwambia hiyo si hoja kama kuna matatizo yanayohusu mastakimu yako ni bora kuandika kwa Mkurugenzi tukaweza kuyazingatia hasa kama ikiwa ni *special conditions* za kukusaidia.

Lakini kuna nyumba ambayo anastahiki kukaa na kubwa litakuja, kwa sababu kawaida mtu anafanya kazi masaa 8, sawa ukiwa nyumbani unaweza kuitwa saa 10. Mhe. Spika, kwa kuwa yeye yupo peke yake inabidi afanye masaa zaidi na itabidi awe analipwa *overtime*, ambalo nalo tayari tumeshalizungumza.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, malizia.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nakushukuru na mengi yatakuja wakati tunapopitisha vifungu.

Lakini naomba nimalizie Mhe. Spika, kwa kutoa shukrani zangu za dhati na wapo wengine wameleta kwa maandishi na mambo yalikuwa yanaingiliana. Kwa hivyo, naomba wanisamehe kwamba sikuweza kumjibu mmoja mmoja, lakini nadhani yale niliyoweza kujibu nimejibu.

Mhe. Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano yenu pamoja na michango yenu, pia nawashukuru wafanyakazi wa Wizara ya Afya, namshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Afya pamoja na wengine wote wanaofanya kazi Wizara ya Afya katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nategemea bajeti hii Waheshimiwa Wajumbe wataipitisha, tumesikia maoni, mashaka yenu na nimeweza kujieleza nilivyoweza kujieleza na mambo mengine yako kwenye *pipeline* na siwezi kuyasema.

Lakini tumeahidiwa misaada ya aina mbali mbali kutoka Ubalozi wa *UAE* yanayohusu mambo ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, ambapo mwenyewe amekuja Balozi ametembelea akaenda akaiona, tumepeleka *document* kubwa tu, ambayo inaonesha *comprehensive requirement*. Vile vile Serikali ya India ambayo ilikubali ambayo ingeweza kutukopesha dola milioni 50 na suala hilo liko kwenye *pipeline* na linategemewa linaweza kukubalika, kwa sababu kuna dalili fulani.

Sasa kama haya yote ambayo yako kwenye *pipeline* nayo yatapatikana, basi mambo mengi ambayo tunayoyalalamikia yanaweza yakapungua.

Mhe. Spika, nakushukuru tena kwa kuniruhusu na kunistahamilia. Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuwashukuru tena na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe.Spika: Mhe. Waziri, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kufanya majumuisho pamoja na Naibu Waziri wako pamoja na mawaziri wote ambao wamesaidia katika kutoa majumuisho ya hoja hii.

Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya makadirio haya wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wetu sio mzuri na ilivyo hoja hii tuimaliza asubuhi hii na kwa kawaida tukiachia hapa basi jioni hatuipitishi tutachelewa. Kwa hivyo, naomba mukubali nitumie *quorum* hii, kwa ajili ya kuimaliza kazi hii. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa kuwa kazi iliopo mbele yetu bado ni kubwa, na kwa kuwa muda wetu kwa mujibu wa Kanuni umeshakaribia kufika wa kusitisha kikao chetu hivi sasa. Kwa hivyo, Mhe. Spika naomba kutoa hoja kwamba tuweke Kanuni kando, ili tuweze kuendelea na majadiliano hadi tumalize shughuli iliopo mbele yetu. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuzingatia niliyoyaeleza niwahoji basi wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokataa wameshinda. *(Vicheko/Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kukataliwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa waliokataa wameshinda na muda uliobaki ni mdogo basi tukubaliane jambo moja. Kwa hivyo, tukubaliane kwamba *quorum* hii tuitake saa 11:00 jioni na nilitaka tuitumie hii, ili tuweze kuendeleza shughuli zetu. Lakini mumekataa kumaliza shughuli hii na mnasema tuje jioni. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, tuji-*commit* kwa kufuata utaratibu wa Kanuni kuingia saa 11:00 hapa, ili tuifanye kazi hii. Kwa kweli mambo haya lazima yatizame pande zote mbili, kwamba Wajumbe tuwe tunakubaliana kufanya kazi zetu kwa mujibu wa taratibu na sio kwamba kila mmoja aje kwa wakati aa! Huo si utaratibu tuliokubaliana. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, saa 11:00 tujeni kama hivi kwa ajili ya kuendeleza kazi hii na baadaye tumuombe Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto asome hoja yake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa muda ni mfupi hatuwezi tukaendelea na jambo lolote pamoja na kwamba mumekataa. Kwa hivyo, naakhirisha kikao hichi hadi saa 11:00 jioni leo. *(Vicheko/Makofi)*

(Saa 6:45 mchana Baraza liliakhirishwa
mpaka saa 11:00 jioni)